

# KATIBA: NGUZO YA UWAJIBIKAJI NA ULINZI WA HAKI

## MUHTASARI WA RIPOTI YA HAKI ZA BINADAMU 2023- TANZANIA BARA

LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE
LHRC
KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Zanzibar Fighting Against Youth Challenges Organization
ZAFAYCO

HAKIUZWI

**Mwandishi, Wahariri, na Mchapishaji**

**Mwandishi:**
Bw. Fundikila Wazambi

**Wahariri:**
Dkt. Anna Henga
Bw. Ally Seif

**Mchapishaji:**
Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu
Machi 2024

**Wadau wa Maendeleo:**

Sweden Sverige

Norwegian Embassy

Ambasáid na hÉireann | Tanzania
Embassy of Ireland | Tanzania
Ubalozi wa Ireland | Tanzania

Wellspring Philanthropic Fund

HAKIUZWI

ISBN: 978-9987-740-71-0
@LHRC 2024

# YALIYOMO


**KUHUSU KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU** ii

**MASUALA MAKUU YALIYOTOKEA MWAKA 2023** iii

**DONDOO MUHIMU** vi

**SURA YA KWANZA:** UTANGULIZI **01**

**SURA YA PILI:** HAKI ZA KIRAIA NA KISIASA **09**

**SURA YA TATU:** HAKI ZA KIUCHUMI,KIJAMII, NA KIUTAMADUNI **28**

**SURA YA NNE:** HAKI ZA KIUJUMLA **39**

**SURA YA TANO:** HAKI ZA MAKUNDI MAALUM **45**

**SURA YA SITA:** VYOMBO VYA ULINZI WA HAKI ZA BINADAMU **60**

**SURA YA SABA:** UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO **62**

# KUHUSU KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ni shirika binafsi, huru, la hiari, lisilo la kiserikali, lisilofungamana na chama chochote cha kisiasa na lisilotengeneza faida kwa ajili ya kugawana, ambalo linalenga kufikia jamii yenye haki na usawa. LHRC ina lengo la kuwawezesha Watanzania kukuza, kuimarisha na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini. Lengo kubwa la LHRC ni kujenga ufahamu wa sheria na haki za binadamu miongoni mwa umma na hasa watu walio katika hatari kubwa ya haki zao za msingi kukiukwa, kutoa elimu ya sheria na uraia, kufanya utetezi unaohusisha pia msaada wa kisheria, pamoja na kufanya utafiti na ufuatiliaji wa haki za binadamu. LHRC ilianzishwa mwaka 1995 na inafanya kazi Tanzania Bara.

# MASUALA MAKUU YALIYOTOKEA MWAKA 2023

- Viashiria vya rushwa, ubadhirifu, na matumizi mabaya ya fedha za umma kuibuliwa katika ripoti za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zilizotoka Mwezi Machi 2023
- Marekebisho ya Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016
- Kutolewa kwa Ripoti ya Kikosi Kazi cha Rais kuhusu Haki Jinai
- Maamuzi ya Makahama ya Haki ya Afrika Mashariki kuhusu watumishi wa Serikali kuwa wasimamizi wa uchaguzi
- Hukumu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kuhusu dhamana
- Hukumu ya Mahakama Kuu kuhusu wagombea nafasi za uongozi kupita na kushinda bila kupingwa
- Mapitio ya sera ya zamani na uletwaji wa Sera Mpya ya Elimu na Mafunzo
- Uondoaji wa kifurushi cha bima ya afya cha Toto Afya
- Uanzishwaji wa Mtandao wa Kupinga Usafirishaji Haramu wa Binadamu Tanzania
- Uondoaji wa katazo la kufanya mikutano ya siasa
- Utungwaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote
- Uanzishwaji na utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia

# DONDOO MUHIMU

| | | |
|---|---|---|
| 1 | **Mauaji yanayotokana na Ukatili dhidi ya Mwenza** | • Matukio zaidi yaliripotiwa mwaka 2023.<br>• Yanasababishwa na ukatili dhidi ya mwenza, ambayo yameendelea kuwa changamoto kubwa.<br>• Yaathiri zaidi haki ya kuishi, haki ya afya, haki ya kuwa salama, na uhuru dhidi ya ukatili.<br>• Asilimia kubwa ya waliofanyiwa ukatili huo (asilimia 90) walikuwa ni wanawake.<br>• Kuna hofu kwamba matukio mengi zaidi yametokea ila hayajaripotiwa. |
| 2 | **Ukatili dhidi ya wanawake & Watoto** | • Ukatili wa kingono dhidi ya watoto (ubakaji na ulawiti) bado ni tishio kubwa kwa haki za watoto.<br>• Ukatili wa kimwili ni changamoto kubwa zaidi kwa wanawake, hasa wale waliokuwa kwenye mahusiano, ikiwemo ya ndoa.<br>• Ukatili wa kiuchumi pia bado ni changamoto kwa wanawake na wasichana: Ni pamoja na kunyimwa haki za kumiliki na kurithi mali; kunyimwa haki na fursa ya elimu kwa wavulana na wasichana; kunyimwa fursa ya kutumia kipato cha familia, hasa maeneo ya vijijini; na uondoaji wa kinguvu wa wajane kwenye nyumba zao, hasa unaofanywa na ndugu wa marehemu waume zao. |
| 3 | **Haki Jinai** | • Tume ya Rais ya Kuboresha Mfumo wa Haki Jinai illibua matatizo na changamoto nyingi katika mnyororo wa haki jinai.<br>• Matumizi ya nguvu kupita kiasi wakati wa kukamata watuhumiwa ni changamoto kubwa.<br>• Hatua za haraka, ikiwemo za kurekebisha sheria, zinahitajika kutatua na kupunguza changamoto za haki jinai, ikiwemo rushwa, ucheleweshaji katika ufanyaji upelelezi na uwekaji kuzuizini wa watuhumiwa kwa muda mrefu. |
| 4 | **Ukatili dhidi ya wazee** | • Wazee, wanaume kwa wanawake, walifanyiwa vitendo mbalimbali vya ukatili wa kimwili, kingono, kisaikolojia, na kiuchumi.<br>• Baadhi ya wazee wanashambuliwa na kuuawa kwa tuhuma za uchawi na sababu ya mali.<br>• Matukio zaidi ya ukatili dhidi ya wazee yaliripotiwa ukilinganisha na mwaka 2022. |

| | | |
|---|---|---|
| **5** | **Upatikanaji wa huduma bora za afya** | • Ulielezewa kuwa changamoto kwa wazee, pamoja na uwepo wa sera ya utoaji wa huduma hizo kwa wazee bure.<br>• Ufinyu wa bajeti na upungufu wa upungufu wa wafanyakazi katika sekta ya afya pia vinaathiri utekelezaji madhubuti wa haki ya afya.<br>• Changamoto katika utoaji wa huduma bora za afya ya mama, ikiwemo upungufu wa wodi za wazazi na utelekezaji unaofanywa na manesi.<br>• Changamoto nyingine ya kiafya, hususan kwa wanawake na wasichana, hasa wanaoishi maeneo ya vijijini, ni afya ya hedhi na hedhi salama.<br>• Kukua kwa tatizo la afya ya akili, linalochangia watu kufanya ukatili na kujitoa uhai. |
| **6** | **Mauaji yanayotokana na imani za kishirikina** | • Huwalenga zaidi watu wa aina na umri fulani na hufanywa na mtu mmoja mmoja au kikundi cha watu, ikiwemo wanafamilia na ndugu wa karibu.<br>• Walengwa wakuu ni wazee, hasa wanawake, ambapo hushambuliwa, kudhalilishwa, na wakati mwingine kuuawa sababu ya tuhuma za uchawi.<br>• Mauaji yamekuwa yakichochewa na waganga wa kienyeji, hasa kupitia utamaduni wao wa kupiga ramli.<br>• Mkoani Kigoma, aliripotiwa mganga maarufu kama 'Kamchape,' ambaye alikuwa anafanya kazi ya 'kufichua' wachawi na 'kuwawajibisha.' |
| **7** | **Athari za mabadiliko ya tabianchi** | • Mabadiliko ya tabianchi yaliathiri makazi, mazingira, na haki za binadamu kwa ujumla kwa namna mbalimbali, ikiwemo mafuriko, uharibifu wa nyumba na miundombinu, ukame, na upunguaji wa uzalishaji.<br>• Haki zilizoathiriwa ni pamoja na haki ya kuishi, haki ya kuishi katika hali inayofaa (haki ya chakula na haki ya makazi), haki ya afya, haki ya maji safi na salama, haki ya mazingira safi na salama, na haki ya maendeleo.<br>• Uelewa wa wanajamii wengi kuhusu mabadiliko ya tabianchi na athari zake pia bado upo chini kwa kiasi kikubwa. |

| | | |
|---|---|---|
| **8** | **Utesaji** | • Kuongezeka kwa matukio ya utesaji.<br>• Matukio hayo ni pamoja na yaliyotokea kwa Wamasai Wilayani Ngorongoro.<br>• Utesaji wa watoto na watuhumiwa walio chini ya ulinzi wa maofisa wa vyombo vya dola pia ni changamoto kubwa. |
| **9** | **Rushwa na usamizi mbaya, matumizi mabaya, na ubadhirifu wa fedha za umma** | • Kwa mara nyingine, ripoti za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ziliibua viashiria vya rushwa na matumizi yasiyo na tija ya fedha za umma.<br>• Matokeo ya utafiti wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yanaonesha tatizo kubwa na ukosefu wa uwajibikaji wa kutosha wa watu na taasisi katika matumizi ya fedha za umma.<br>• Haki ya maendeleo iliathiriwa zaidi, hasa kwa upande wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.<br>• Fedha zilizopotea zingeweza kuimarisha zaidi utekelezaji wa haki za kiuchumi na kijamii. |
| **10** | **Haki ya kumiliki mali** | • Ufurahiaji na utekelezaji wa haki ya kumiliki mali uliathiriwa na migogoro ya ardhi iliyotokea katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara.<br>• Wafugaji pia walilalamika kuhusu ukiukwaji wa haki yao ya kumiliki mali na kuitaka Serikali ifanye marekebisho ya sheria kulinda haki hiyo ya kikatiba.<br>• Sheria za kimila zimeendelea kuwa kikwazo kikubwa kwa haki za wanawake na wasichana za kumiliki na kurithi mali.<br>• Haki ya wazee ya kumiliki mali pia ilikiukwa, hasa na watoto wao. |
| **11** | **Bima ya afya** | • Kutungwa wa sheria ya bima ya afya kwa wote, kukileta matumaini mapya katika ulinzi na utekelezaji wa haki ya afya. |

# MAPENDEKEZO MAKUU

| | |
|---|---|
| **Marekebisho ya sheria, ikiwemo katika mfumo wa haki jinai** | Sheria ambazo zinahitaji kufanyiwa marekebisho kulinda haki za binadamu ni pamoja na: Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015; Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016; Kanuni za Maudhui Mtandaoni za mwaka 2020; Sheria ya Utekelezaji wa Haki na Wajibu wa Msingi (BRADEA), iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2021; sheria za kimila (kulinda haki za wasichana na wanawake kumiliki na kurithi mali); sheria zote za uchaguzi (kuboresha na kuweka vifungu kuhusu masuala ya jinsia na kuimarisha ushiriki katika siasa); na Sheria ya Vyama vya Uchaguzi kulinda zaidi uhuru wa vyama vya siasa wa kujumuika na kukusanyika. |
| **Wadau wa kiserikali na wasio wa kiserikali pamoja na watu wengine kutoingilia haki za binadamu kinyume na sheria, hasa haki za kiraia na kisiasa** | |
| **Katiba mpya** | Hii inahitajika ili kuimarisha ulinzi wa haki za binadamu. |
| **Tanzania kuridhia mikataba mbalimbali kuhusu haki za binadamu ambayo bado haijaridhia** | Mikataba hiyo ni pamoja na: Mkataba wa Afrika wa Demokrasia, Uchaguzi, na Utawala wa mwaka 2007; Mkataba wa Pili wa Nyongeza kwenye Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa kuhusu Ufutaji wa Adhabu ya Kifo; Mkataba dhidi ya Utesaji na Adhabu au Vitendo vingine vya Kikatili, visivyo vya Kibinadamu, vya Kinyama na vyenye Kudhalilisha wa Mwaka 1984 (Mkataba dhidi ya Utesaji); na Mkataba wa Umoja wa Afrika kuhusu Usalama Barabarani wa mwaka 2016. |
| **Utekelezaji wa sheria, kanuni, na sera kuhusu ulinzi wa haki za binadamu** | |
| **Utungwaji wa sheria za kulinda makundi maalum** | Sheria hizo ni sheria ya ulinzi wa haki za wazee na sheria ya kupinga ukatili wa kijinsia. Kuna haja ya wadau mbalimbali, zikiwemo asasi za kiraia, kuendelea kufanya uchechemuzi, ikiwemo kupitia kampeni mbalimbali, wazee waweze kuletewa pensheni ya kila mwezi. |

| | |
|---|---|
| **Utekelezaji wa hukumu za mahakama** | Hukumu hizo ni pamoja na hukumu mbalimbali ambazo zimetolewa na mahakama za nchi pamoja na mahakama za kikanda, ikiwemo kuhusu adhabu ya kifo, ndoa za utotoni, mgombea binafsi, na kuhoji matokeo ya uchaguzi wa rais mahakamani. |
| **Kuhakikisha maofisa wa vyombo vya dola wanaokiuka haki za binadamu wanawajibishwa.** | |
| **Kuongeza bajeti za sekta muhimu kama vile elimu, afya, maji, na kilimo, kulingana na viwango vya kimataifa** | |
| **Kutatua changamoto mbalimbali ambazo vyombo vya ulinzi wa haki za binadamu vinakabiliana nazo** | |
| **Kutenga rasilimali za kutosha, ikiwemo bajeti, kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto** | |
| **Kuongeza uelewa wa umma kuhusu haki za binadamu** | |
| **Serikali kufanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti za Mkaguzi Mkuu wa Serikali, Ripoti ya Kikosi Kazi cha Rais kuhusu Demokrasia ya Vyama VIngi, na Ripoti ya Tume ya Rais kuhusu Maboresho ya Mfumo wa Haki Jinai nchini** | |



01


Sura ya Kwanza

# UTANGULIZI

# SURA YA KWANZA:
# UTANGULIZI

## 1.1.Historia Fupi

Kabla ya kupata uhuru miaka ya 1961 (Tanganyika) na 1963 (Zanzibar), Tanzania ilikuwa chini ya tawala za kikoloni za Kijerumani, Kiingereza, na Kiarabu, ambazo ziliambatana na ukiukwjai mkubwa wa haki za wazawa. Ni ukiukwaji huu mkubwa wa haki za binadamu ndiyo ulipelekea wazawa toka pande zote mbili za muungano (Tanganyika na Zanzibar) kupambana, kudai, na hatimaye kupata uhuru. Baada ya uhuru, Tanzania, ambayo ilipatikana baada ya muungano wa nchi za Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964, haikupiga hatua sana katika ulinzi na ukuzaji wa haki za binadamu hadi ilipofika mwaka 1984 yalipotokea mabadiliko ya kikatiba. Kutokana mabadiliko haya ya kikatiba, Muswada wa Haki za Binadamu uliingizwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ukianishwa haki za msingi za binadamu kuanzia Ibara ya 12 hadi 24. Hatua hii muhimu, ambayo ilifikiwa katika katiba ya tano tangu kupata uhuru, ilikuwa ni mwanzo wa safari ya ulinzi madhubuti zaidi wa haki za binadamu nchini na ilichochea mabadiliko ya kikatiba ya mwaka 1992 yaliyoleta demokrasia ya vyama vingi sambamba na kuanzishwa kwa mashirika yasiyo ya kiserikali yanayofanya uchechemuzi wa haki za binadamu katika miaka ya 1990 na 2000.




## 1.2. Idadi ya Watu

Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi iliyofanyika mwaka 2022, kwa sasa idadi ya watu nchini Tanzania ni 61,741,120, ambapo kati

yao aslimia 51 ni wa kike na asilimia 49 ni wa kiume. Asilimia 96.9 ya watu wapo Tanzania Bara na asilmia 3.1 iliyobaki wapo Zanzibar. Idadi kubwa ya watu ipo maeneo ya vijijini, ambapo pia idadi ya kaya ni kubwa zaidi ukilinganisha na maeneo ya mjini.

## 1.3.Mihimili ya dola na wajibu wa mihimili hiyo katika ulinzi wa haki za binadamu

Kuna mihimili mikuu mitatu ya dola nchini Tanzania, ambayo ni: Serikali, Bunge na Mahakama. Mihimili hii imeanzishwa na kupewa mamlaka na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

### *A. Serikali Kuu*

Serikali inajumuisha Rais - ambaye ni Kiongozi wa Taifa, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu - na Baraza la Mawaziri. Baraza la mawaziri linajumuisha Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Rais wa Zanzibar, na mawaziri wote. Rais ndiye Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri. Makamu wa Rais anamsaidia Rais kwenye mambo yote ya muungano. Zanzibar ina serikali yake na Rais wake chini ya mfumo wa serikali mbili ambao Tanzania inautumia, na ina mamlaka juu ya mambo yote ambayo siyo ya muungano, kama yalivyoainishwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

***Wajibu katika ulinzi wa haki za binadamu:***
Wajibu wa Serikali Kuu ni pamoja na kutekeleza majukumu yake chini ya mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imeridhia; kuilinda Katiba, ambayo inajumuisha haki za binadamu; kuhakikisha utekelezaji wa haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni kwa kutoa huduma za kijamii kama vile maji, afya na elimu; kulinda haki ya kuwa huru na salama kupitia vyombo vya dola na mifumo ya haki; na kutoa ulinzi wa kisheria na wa haki za binadamu kupitia Jeshi la Polisi, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, na wizara husika katika sekta mbalimbali.

| Marais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
|---|
| Mw. Julius Kambarage Nyerere: 1964-1985 |
| Ali Hassan Mwinyi: 1985-1995 |
| Benjamin William Mkapa: 1995-2005 |
| Jakaya Mrisho Kikwete: 2005-2015 |
| John Pombe Magufuli: 2015- 2021 |
| Samia Suluhu Hassan – 2021 mpaka sasa |

### *B.Bunge*

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo chombo kikuu cha kutunga sheria nchini, ambacho kinaundwa na wabunge mbalimbali wa chama tawala na vyama vya upinzani. Rais pia ni sehemu ya Bunge kwa mujibu wa Katiba. Kazi kuu ya bunge ni kuisimamia na kuishauri Serikali. Bunge

hili lina mamlaka juu ya mambo yote ya muungano. Zanzibar ina Baraza la Wawakilishi, ambalo ndiyo chombo chake kikuu cha kutunga sheria na kuisimamia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Bunge lina wabunge wa kuchaguliwa na wabunge wa kuteuliwa.

***Wajibu katika ulinzi wa haki za binadamu:*** Utungaji wa sheria za kulinda haki za binadamu; uridhiaji wa mikataba na utungaji wa sheria za kusaidia utekelezaji wa mikataba hiyo; kuisimamia na kuishauri Serikali katika utekelezaji wa shughuli zake; kujadili masuala mbalimbali yanayohusiana na haki za binadamu na kuyatolea maamuzi.

### C.Mhimili wa Mahakama

Mahakama ni chombo kikuu cha utoaji haki nchini Tanzania, ambapo kuna mahakama kadhaa ambazo zinatofautiana kimamlaka. Mahakama ya juu kabisa ni Mahakama ya Rufani, ambayo ina Majaji wa Mahakama ya Rufani, ambao husimamia na kutolea maamuzi kesi zote za rufaa. Ya pili ni Mahakama Kuu, ambayo pia ina majaji (Majaji wa Mahakama Kuu), ambao husimamia kesi zote katika ngazi hiyo na kuzitolea maamuzi. Mahakama zinazofuatia ni Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Mwanzo – ambayo ndiyo mahakama ya chini kabisa. Tofauti na Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu, mahakama hizi za chini zina mahakimu. Mahakama Kuu ina vitengo mbalimbali, ikiwemo cha ardhi, biashara, kazi, na cha rushwa – ambacho kiliundwa mwaka 2016. Majaji wanateuliwa na Rais baada ya kupata ushauri wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, huku mahakimu wakichaguliwa na Tume hiyo moja kwa moja. Pia kuna Mahakama Maalum ya Katiba, ambayo ina mamlaka ya kushughulikia kesi za kikatiba, ikiwemo haki za binadamu. Ukiacha mahakama hizi, kuna mahakama za kijeshi-ambazo ni mahsusi kwa ajili ya wanajeshi.

Mahakama ya Rufani ni mahakama yenye mamlaka hadi Zanzibar, ambayo pia ina mahakama zake ziitwazo Mahamaka Kuu ya Zanzibar, Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Mwanzo. Pia kuna Mahakama ya Rufani ya Kadhi na Mahakama ya Kadhi.

***Wajibu katika ulinzi wa haki za binadamu:*** Mhimili huu una wajibu mkubwa katika ulinzi wa haki za binadamu, ikiwemo kutafsiri sheria mbalimbali, ikiwemo zinazohusu haki za binadamu; kuchukua hatua za kisheria dhidi ya watuhumiwa wa vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu; na kusikiliza madai yanayohusiana na haki za binadamu. Mhimili huu pia hufanya mapitio ya maamuzi

na vitendo vya watu na mamlaka mbalimbali kulingana na viwango vya haki za binadamu; huimarisha upatikanaji wa haki; hukuza utaratibu wa kisheria; na hutunga au kufanunua sheria kupitia kesi.

### 1.4.Kuhusu Ripoti

Ripoti ya Haki za Binadamu ya Mwaka 2023 ni ripoti ya 22 ya haki za binadamu kuandaliwa na LHRC tangu shirika lilipoanzisha utaratibu huo mwaka 2002. Ripoti ya mwaka huu imeangazia hali ya haki za binadamu kwa pande zote mbili za Tanzania Bara na Zanzibar, ambapo Sehemu ya Kwanza imejikita kwa Tanzania Bara na Sehemu ya Pili imejikita Zanzibar. Ripoti ni matokeo ya tathmini ya hali ya haki za binadamu nchini iliyofanywa kulingana na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu, na inajumuisha vizazi vyote vitatu vya haki za binadamu, ambavyo ni: haki za kiraia na kisiasa; haki za kiuchumi, kijamii, na kiutamaduni; na haki za kiujumla.

## 1.5. Madhumuni ya Ripoti na Ukusanyaji Data na Taarifa

**MADHUMUNI**

**Elimu ya haki za binadamu** – haki fulani inamaanisha na kujumuisha nini? Haki hiyo inalindwa na mfumo upi wa kisheria? Kwa nini haki hii ni muhimu? Haki hii ina mipaka ipi?
**Kukumbushia** – ni maeneo gani ya haki za binadamu yanahitaji kuimarishwa?
**Uchechemuzi wenye ushahidi** – nini kinahitaji kubadilika na kwa nini?
**Mambo na matukio yaliyosaidia ulinzi na utekelezaji wa haki za binadamu** – ni mambo au matukio gani yameimarisha ulinzi au utekelezaji wa haki za binadamu?
**Mambo na matukio yaliyoathiri ulinzi na utekelezaji wa haki za binadamu** – ni mambo au matukio gani yameathiri ulinzi na utekelezaji wa haki za binadamu?
**Uchambuzi wa sheria na miswada** – ni nini kimebadilika kufuatia utungwaji wa sheria au marekebisho ya sheria au kanuni? Mabadiliko hayo yameleta au yataleta athari gani kwenye haki za binadamu?
**Mapendekezo** – nini kifanyike kuimarisha na kulinda haki za binadamu?
**Utoaji taarifa** – kutoa taarifa kuhusu haki za binadamu na masuala ya kisheria ili kuchukua tahadhari na kutekeleza wajibu wako kwa mujibu wa sheria mbalimbali za nchi.
**Kuonyesha mienendo** – hali ilikuwaje miaka ya nyuma ukilinganisha na sasa?
**Kutoa mwanga katika kupanga afua** – ripoti inaweza kutumika kama sehemu ya kuanzia katika kupanga afua mbalimbali.
**Kuelemisha** – kutoa elimu kuhusu haki za binadamu; elimu kuhusu mifumo ya ulinzi wa haki za binadamu ya kitaifa, kikanda na kimataifa; elimu kuhusu masuala ya kisheria; elimu kuhusu mambo mapya kuhusu sheria na haki za binadamu.

## UKUSANYAJI DATA NA TAARIFA

Data na taarifa zilizotumika kuandaa Ripoti hii zilipatikana kupitia vyanzo vya awali na upili. Data na taarifa za awali zilipatikana kupitia Utafiti wa Haki za Binadamu 2023, ambao ulifanyika katika mikoa 20 ya Tanzania Bara, na programu za kituo, hasa programu za msaada wa kisheria na ufuatiliaji wa haki za binadamu. Data na taarifa za upili zilipatikana kupitia mapitio ya vyanzo mbalimbali vya kuaminika vya habari na taarifa, ikiwemo ripoti za wadau wa kiserikali na wasio wa kiserikali, hotuba, na matamko mbalimbali. Pia, utafiti wa LHRC wa taarifa zilizotolewa na vyombo vya habari kwa mwaka 2023 ulitoa data na taarifa muhimu zilizosaidia uandaaji wa ripoti hii ya haki za binadamu, sambamba na kuwezesha ufanyaji wa utafiti zaidi kuhusu masuala mbalimbali yanayohusiana na sheria na haki za binadamu yaliyojitokeza katika taarifa hizo.

### 1.6. Muhtasari wa Hali ya Haki za Binadamu kwa mwaka 2023

Kulingana na tathmini ya hali ya haki za binadamu nchini iliyofanywa na LHRC kwa kutumia viwango vya kimataifa vya haki za binadamu, kwa ujumla hali ya haki za binadamu nchini ilidorora kiasi mwaka 2023 ikilinganishwa na mwaka 2022.

#### Masuala ya haki za binadamu yaliyoripotiwa zaidi

Kama ilivyokuwa katika mwaka 2022, masuala mengi kuhusu haki za binadamu yaliyoripotiwa mwaka 2023 yalikuwa ni ya ukiukwaji wa haki za kiraia na kisiasa, ikiwemo uhuru dhidi ya ukatili. Matukio mengi ya aina mbalimbali za ukatili dhidi ya wanawake, watoto, watu wenye ulemavu, na wazee yaliripotiwa katika sehemu mbalimbali nchini. Matukio hayo yalipelekea kutokea kwa aina mbalimbali za mauaji, ikiwemo mauaji yanayofanywa na mwenza dhidi ya mwenza na mauaji yanayotokana na imani za kishirikina. Hali kadhalika, matukio hayo yalipelekea unyimwaji wa haki za kumiliki na kurithi mali pamoja na kusababisha madhara ya kimwili na kisaikolojia. Pia, masuala ya haki jinai yaliripotiwa na kujadiliwa sana mwaka 2023, ikiwemo watuhumiwa wengi kuendelea kusota gerezani sababu ya mapungufu katika mfumo wa haki jinai. Matukio ya utesaji pia yaliripotiwa katika sehemu mbalimbali ya Tanzania Bara.

## Haki zilizokiukwa zaidi

**1. Haki ya kuishi**

*[Mauaji yanayotokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi; Mauaji yanayotokana na imani za kishirikina; Mauaji ya wazee; Mauaji yanayofanywa na mwenza dhidi ya mwenza]*

**2. Uhuru dhidi ya Ukatili**

*[Ukatili dhidi ya watoto, hasa wa kingono; Ukatili dhidi ya mwenza; Ukatili dhidi ya watu wenye ulemavu na wazee; Ukatili wa kimwili na kiuchumi dhidi ya wanawake]*

**3. Haki ya Usawa mbele ya Sheria**

*[Kuwekwa kuzuizini kwa muda mrefu; Vikwazo vya ufikiaji haki m.f. rushwa]*

**4. Haki ya kuwa Huru na Salama**

*[Uwekwaji kuzuizini gerezani kwa muda mrefu kusubiria kesi; Kunyimwa dhamana; Ukatili dhidi ya wanawake, watu wenye ulemavu, na watoto; Ukamataji na uwekaji kuzuizini watu kinyume na sheria; Ubambikaji wa kesi]*

**5. Uhuru dhidi ya Mateso**


*[Utesaji wa watuhumiwa walio chini ya ulinzi;utesaji wa watoto; utesaji kutumika kama adhabu]*

## Masuala mengine muhimu ya haki za binadamu

Kwa mwaka 2023, masuala mengine muhimu yaliyotokea ni pamoja na mauaji yanayotokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi, mauaji yanayotokana na imani za kishirikina, ukatili dhidi ya mwenza, mauaji yanayofanywa na mwenza dhidi ya mwenza, ukiukwaji wa haki za mtuhumiwa (ikiwemo sababu ya kuwekwa kizuizini kwa muda mrefu), usafirishaji haramu wa binadamu (ikiwemo watoto), ajira kwa watoto, ndoa za utotoni, faragha na ulinzi binafasi, ukeketaji, bima ya afya, na ukiukwaji wa haki za kumiliki mali na kurithi (hususan kwa wanawake, wakiwemo wajane).

## Manusura wa ukiukwaji wa haki za binadamu

Kulingana na matukio ya ukiukwaji wa haki za binadamu yaliyokusanywa na LHRC mwaka 2023, watoto waliendelea kuongeza kwa idadi ya manusura (45%), wakifuatiwa na wanawake (30%), wazee (12%), wanaume (10%), na watu wenye ulemavu (3%).




*Manusura wa ukukwaji wa haki za binadamu kulingana na matukio yaliyokusanywa na LHRC mwaka 2023*

## 1.7.Muundo wa Ripoti

| | |
|---|---|
| **Sura ya 1 Utangulizi** | Inaelezea kwa kifupi kuhusu Tanzania na kuelezea kwa kifupi kuhusu uandaaji, madhumuni, na muundo wa ripoti. |
| **Sura ya 2 Haki za Kiraia na Kisiasa** | Inaelezea hali ya haki za msingi za kiraia na kisiasa, ikiwemo uhuru wa kujumuika na kukusanyika; uhuru wa kujieleza; haki ya usawa mbele ya sheria na kupata nafuu ya kisheria; na haki ya kuishi. |
| **Sura ya 3 Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni** | Inaelezea haki muhimu za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni, ikiwemo haki ya kufanya kazi, haki ya elimu, haki ya afya, haki ya maji safi na salama, haki ya kumiliki mali, na haki ya kuishi katika hali inayofaa. |
| **Sura ya 4 Haki za Kiujumla** | Inaangazia hali ya haki za kiujumla, hususan haki ya maendeleo, haki ya kufurahia na kufaidika na rasilimali asilia, na haki ya mazingira safi na salama |
| **Sura ya 5 Haki za Makundi Maalum** | Inaelezea hali ya haki za makundi maalum, ikiwemo wanawake, watoto, watu wenye ulemavu, na wazee. |
| **Sura ya 6 Vyombo vya Ulinzi wa Haki za Binadamu** | Inaangazia vyombo ya ulinzi wa haki za binadamu katika ngazi za kitaifa, kikanda, na kimataifa na kujadili wajibu wake katika ulinzi wa haki za binadamu. |
| **Sura ya 7 Utekelezaji wa Mapendekezo** | Inafanya tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti zilizopita za haki za binadamu |



02

Sura ya Pili

# HAKI ZA KIRAIA NA KISIASA

## SURA YA PILI:
# HAKI ZA KIRAIA NA KISIASA

Haki za kiraia na kisiasa zilizojadiliwa katika sura hii ni haki ya kuishi, uhuru wa kujieleza, uhuru wa kujumuika, uhuru wa kukusanyika, haki ya usawa mbele ya sheria, haki ya nafuu madhubuti ya kisheria, haki ya kuwa huru na salama, haki ya kushiriki katika utawala, uhuru dhidi ya utesaji na kutendewa kama siyo binadamu, uhuru dhidi ya ukatili, na haki ya faragha.


Kwa mwaka 2023, masuala makuu yaliyoathiri ufurahiaji wa haki za kiraia na kisiasa ni pamoja na mauaji, ukiukwaji wa uhuru wa vyombo vya habari, ukatili, vikwazo vya upatikanaji haki, na changamoto za haki jinai.

### 2.1. Haki ya Kuishi

Kwa mwaka 2023, haki ya kuishi kwa upande wa Tanzania Bara iliendelea kukiukwa kwa njia mbalimbali, ikiwemo mauaji yanayotokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi, mauaji yanayotokana na maofisa wa vyombo vya habari kutumia nguvu kupita kiasi, mauaji yanayotokana na imani za kishirikina, adhabu ya kifo, mauaji ya waliouwawa na mwenza dhidi ya mwenza, matukio ya watu kupotea, na ajali za barabarani.

#### Mauaji yanayotokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi

Kwa mwaka 2023, LHRC ilikusanya matukio 42 ya mauaji yanayotokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi, ambayo ni matukio mawili zaidi ya yale yaliyoripotiwa mwaka 2022. Walioawa walikuwa na kati ya umri wa miaka 15 hadi 40, wengi wao wakiwa vijana. Miongoni mwa waliouawa ni watoto wenye umri wa miaka 15 na 17. Hata hivyo, idadi ya matukio ambayo hukusanywa na LHRC ni sehemu ndogo tu ya matukio ambayo kwa kawaida hukusanywa na Jeshi la Polisi. Takwimu za jeshi hilo zinaonyesha kwamba, tangu mwaka 2020, zaidi ya matukio 400 huripotiwa kila mwaka. Kwa mwaka 2023, matukuio 461 yaliripotiwa polisi.




**Zaidi ya matukio 400 ya mauaji yanayotokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi hutokea kila mwaka.**

**Mtazamo wa LHRC:** Mauaji yanayotokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi yameendelea kuwa tishio kwenye haki za binadamu na yanachangiwa na wananchi kutokuwa na imani na mfumo wa haki jinai kwa sababu mbalimbali, ikiwemo rushwa katika vyombo vya dola na haki, na kutokuwa na uelewa mzuri kuhusu sheria za jinai, ikiwemo suala la dhamana.

**Wito wa LHRC:** LHRC inatoa wito kwa wanajamii kuacha kujichukulia sheria mkononi na kwa mashirika yasiyo ya kiserikali na wadau wengine kuendelea kueneza uelewa kuhusu namna mfumo wa haki jinai unavyofanya kazi pamoja na athari zinazotokea sababu ya wananchi kujichukulia sheria mkononi.

## Mauaji yanayotokana na maofisa wa vyombo vya dola kutumia nguvu kupita kiasi na ukatili unaofanywa dhidi ya maofisa wa vyombo hivyo

### Mauaji yanayotokana na maofisa wa vyombo vya dola kutumia nguvu kupita kiasi

Mauaji yanayotokana na maofisa wa vyombo vya dola kutumia nguvu kupita kiasi hutokea pale ambapo maofisa wa dola wametumia nguvu kupitika kiasi kumdhibiti mtuhumiwa na kusababisha kifo chake. Kwa mwaka 2023, LHRC ilikusanya matukio saba (7) ya aina hii ya mauaji, ambayo ni mtukio matatu pungufu ya yale yaliyoripotiwa mwaka 2022. Maofisa wa vyombo vya dola waliohusishwa na mauaji hayo ni pamoja na askari polisi na maofisa wanyamapori. Mojawapo ya matukio ni tukio lilitokea jijini Dar es Salaam mwezi wa Novemba 2023, ambapo maofisa wawili wa polisi walidaiwa kumpiga risasi na kumuua mlinzi wa baa moja ilyopo Wilaya ya Kinondoni. Katika tukio jingine liliripotiwa mkoani Mara mwezi Machi, polisi mmoja wilayani Tarime alikamatwa kwa kumpiga risasi na kumuua dereva bodaboda, Ng'ondi Marwa Masiaga (22), mkazi wa Kijiji cha Kubiterere.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
JESHI LA POLISI TANZANIA



Simu Namba: 028 2690037
Fax: 028 2690125
E – Mail: rpc.tarimerorya@tpf.go.tz

Ofisi ya Kamanda wa Polisi
Mkoa wa Polisi Tarime Rorya
S. L. P 02
**TARIME**

**31.03.2023**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Ndugu Wanahabari,

Leo tarehe 31.03.2023 majira ya 0800hrs huko katika Kitongoji cha Nyansisine Kijiji cha Kubiterere Kata ya Kubiterere Wilaya ya Polisi Sirari, Mkoa wa Polisi Tarime Rorya, kumetokea tukio la Askari namba H.4489 PC KULULETELA wa Kituo cha Polisi Sirari kumfyatulia risasi mwananchi aitwaye NG'ONDI MARWA MASIAGA miaka 22, Mkurya, mfanyabiashara wa bodaboda na mkazi wa mtaa wa Regoryo Tarime.

Ni kwamba Askari huyo kwa uzembe wake mwenyewe na bila uhalali wowote, alimfyatulia risasi raia huyo asiyekuwa na hatia na kumjeruhi kwenye paja lake la mguu wa kulia. Madhura huyo alikimbizwa katika Hospitali ya Wilaya ya Tarime ambapo alifariki dunia akiwa anapatiwa matibabu. Uchunguzi wa awali umebaini kuwa marehemu alifariki kutokana na kupoteza damu nyingi.

Tunamshikilia Askari huyo katika mahabusu ya kituo cha Polisi Tarime. Upelelelezi wa shauri hili unaendelea na utakamilishwa mapema. Mwili wa marehemu umehifadhiwa katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Tarime ukisubiri uchunguzi wa kitabibu.

Niseme kwamba, huyu ni Askari Polisi aliyefunzwa na kufuzu mafunzo yote ya Polisi yakiwemo matumizi sahihi ya silaha. Hivyo alichokifanya ni kinyume na taratibu na sheria za nchi na anastahili kuwajibika kwa hilo.

Ndugu Wanahabari,

Jeshi la Polisi Mkoa wa Polisi Tarime Rorya hatutakuwa na muhali kwa mhalifu yeyote, hivyo askari huyu atachukuliwa hatua kama watuhumiwa wengine.

Asanteni kwa kunisikiliza.

Imetolewa na:

**Kamanda wa Polisi**
Mkoa wa Polisi Tarime Rorya.

***Taarifa ya polisi kwa vyombo vya habari kuhusu askari polisi aliyediawa kumuua mtu wilayani Tarime***

**47**

Idadi ya matukio ya mauaji yanayotokana na maofisa wa vyombo vya dola kutumia nguvu kupita kiasi yaliyokusanywa na LHRC kuanzia mwaka 2017 hadi 2023, mengi yakifanywa na askari polisi, askari wanyama pori, na askari mgambo.

**Wito wa LHRC:** Maofisa wa vyombo vya dola, wakiwemo askari polisi, kutojihusisha na vitendo vya matumizi ya nguvu kupita kiasi na kinyume na sheria ambayo yanapelekea kutokea kwa vifo vya watuhumiwa wa uhalifu. Pia, kuna haja ya kuundwa kwa chombo maalum cha kuchunguza utendaji kazi wa maofisa wa vyombo vya dola, ikiwemo askari polisi, ambacho mojawapo ya kazi zake itakuwa ni kuchunguza tuhuma za mauaji yanayotokana na maofisa wa vyombo vya dola kutumia nguvu kupita kiasi.

### *Ukatili unaofanywa dhidi ya maofisa wa vyombo vya dola*

Kwa mwaka 2023, LHRC ilikusanya tukio moja la ukatili dhidi ya maofisa wa vyombo vya dola ambalo liliripotiwa mkoani Geita. Katika tukio hilo, lilitokea Mwezi Machi wilayani Geita, kikundi cha wananchi wenye hasira kilivamia kituo cha polisi na kukichoma moto baada ya kuwatuhumu maaskari polisi toka kituo hicho kusababisha kifo cha mkazi wa Kijiji cha Mganza, Enos Msalama (34), ambaye alikuwa chini ya ulinzi wa polisi kwa tuhuma za kuiba betri ya gari.

**Wito wa LHRC:** Wananchi kutojihusisha na vitendo vya kuwashambulia maofisa wa vyombo vya dola, kwani kufanya hivyo siyo tu ni kosa kisheria, bali pia ni ukiukwaji wa haki za maofisa hao kama binadamu.

## Mauaji yanayotokana na imani za kishirikina na Ukatili dhidi ya watu wenye ualbino

### *Mauaji yanayotokana na imani za kishirikina*

Mauaji yanayotokana na imani za kishirikina, hasa mauaji ya watu wanaodaiwa kuwa wachawi, yaliendelea kuwa tishio kubwa kwa haki ya kuishi mwaka 2023. Mauaji haya yanachangiwa na imani za kishirikina, ambazo zimeota mizizini Tanzania Bara. LHRC ilikusanya matukio 12 ya mauaji yanayotokana na imani za kishirikina, ambayo ni matukio matano pungufu ukilinganisha na matukio yaliyokusanywa mwaka 2022. Manusura wengi wa aina hii ya mauaji walikuwa wanawake (75%), ikiwemo wanawake wazee. Mojawapo ya matukio ni tukio lilitokea Mwezi wa Februari mkoani Geita, ambapo polisi walimkata bwana mmoja, Juma Charles na mke wake, Joyce Julius, kwa tuhuma za kumuua baba wa mume, Butamo Igonzelo (70), baada ya kumtuhumu kumroga na kumuua mtoto wao wiki moja kabla ya tukio.

Mkoani Kigoma, uliripotiwa uwepo wa mganga wa kienyeji, maarufu ***Kamchampe,*** ambaye alidaiwa kuwasaidia wanajamii kupambana na kuwafichua wachawi wanaowarudisha nyuma kimaendeleo. Iliripotiwa pia kwamba kuna kikosi kazi kimeungwa kuwatafuta na kuwawajibisha watu waliotuhumiwa uchawi na Kamchape, na kwamba kikundi hicho kilishaua watu 'wachawi' wanne.

> **164**
> matukio ya mauaji yanayotokana na imani za kishirikina yaliyoripotiwa polisi mwaka 2023.

Matukio ambayo yanakusanywa na LHRC ni sehemu ndogo tu ya matukio ambayo hukusanywa na Jeshi la Polisi. Mathalani, tangu mwaka 2019, takwimu za polisi zinaonyesha kwamba ***zaidi ya watu 100 wamekuwa wakiuwawa kwa sababu ya imani za kishirikina kila mwaka.***

**Mtazamo wa LHRC:** Imeonekana kwamba mauaji yanayotokana na imani za kishirikina yamekuwa yakichochewa na 'waganga wa kienyeji,' hasa kupitia utaratibu wao wa kupiga ramli kutambua wachawi. Pia, Sheria ya Uchawi, ambayo tuliirithi kutoka kwa wakoloni, imepitwa na wakati, haijasaidia kutatua changamoto, na hivyo ni vyema ikafutwa.

**Wito wa LHRC:** Serikali na wadau wengine, zikiwemo asasi za kiraia, itoe elimu na kueneza uelewa kuhusu imani za kishirikina na mauaji yanayotokana na imani hizo.

### *Ukatili dhidi ya watu wenye ualbino*


Mashambulizi na mauaji ya watu wenye ualbino nchini Tanzania na maeneo mengine barani Afrika yamekuwa yakihusishwa na imani za kishirikina. Hii ni kwa sababu kuna imani imejengeka katika jamii kwamba kiungo cha mwili wa mtu mwenye ualbino kinaweza kutumiwa na wa mganga wa kienyeji kutengeneza dawa ya kumfanya mtu afanikiwe katika mambo yake, ikiwemo kupata utajiri.

Kwa mwaka 2023, LHRC haikukusanya tukio lolote la mashambulizi au mauaji ya watu wenye ualbino kwa sababu ya kupata viungo vyao. Hata hivyo, kwa kiasi kikubwa watu wenye ualbino bado wanaendelea kuishi kwa hofu ya kushambuliwa na hivyo jitihada zaidi zinahitajika kuwafanya wajihisi salama ili waweze kufurahia haki zao za binadamu sawa na watu wengine.

### Adhabu ya kifo

Adhabu ya kifo inakiuka haki ya kuishi na ni ya kikatili na isiyo ya kibinadamu. Hata hivyo, adhabu hii imeendelea kuwa sehemu ya sheria za adhabu nchini Tanzania. Ikumbukwe pia kwamba adhabu hii haijatekelezwa tangu mwaka 1994 chini ya utawala wa Rais Ali Hassan Mwinyi, takribani mika 30 iliyopita!

Kwa mwaka 2023, LHRC ilikusanya matukio 37 ya adhabu ya kifo ambayo ilitolewa na Mahakama Kuu katika maeneo mbalimbali nchini, ambapo karibia watuhumiwa wote waliokutwa na hatia na kuhukumiwa adhabu hiyo (asilimia 94) ni wanaume. Hali kadhalika, adhabu ya lazima ya kifo bado inaendelea kutolewa, kinyume na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu.




***Idadi ya adhabu za kifo zilizokusanywa na LHRC – 2017 hadi 2023***



MWANANCHI

SUPA JACKPOT 1,096,041,286

Pinda: Adhabu ya kifo ifutwe nchini

LHRC yapaza sauti ndoa za utotoni

RC Mara amuonya Mwita Waitara kumkwamisha, alia hadharani

***Habari kuhusu pendekezo la Waziri Mkuu mstaafu kutaka adhabu ya kifo ifutwe nchini (Gazeti la Mwananchi)***

| Mapendekezo ya Tume ya Mabadiliko ya Haki JInai |
| --- |
| • Sheria ya Kanuni za Adhabu (Sura ya 16) irekebishwe kufanya adhabu ya kifo isiwe adhabu pekee kwa waliokutwa na hatia ya mauaji (adhabu ya lazima ya kifo kwa kosa la mauaji).<br>• Adhabu ya kifo ipunguzwe na kuwa kifungo cha maisha pale ambapo Rais hatoidhinisha utekelezaji wa adhabu hiyo ndani ya kipindi cha miaka mitatu. |

**Mtazamo wa LHRC:** LHRC inapendekeza kuondolewa adhabu ya kifo kwa sababu mbalimbali, ikiwemo adhabu ya kifo kuwa ni ya kikatili na ukweli kwamba watu wasio na hatia wamehukumiwa kimakosa adhabu ya kifo katika sehemu mbalimbali duniani lakini adhabu hiyo hairekebishiki. Adhabu ya kifo imeshindwa kufikia lengo lake kuu la kuzuia uhalifu, na hii ni mojawapo ya sababu zaidi ya asilimia 70 za nchi duniani zimeondoa adhabu ya kifo katika sheria au mazoea.

**Wito wa LHRC:** Ikiwa ni miongoni mwa nchi ambazo hazitekelezi adhabu ya kifo, ipo haja ya Tanzania kujiunga na nchi nyingine nyingi duniani na kuchukua hatua ya kuondoa kabisa adhabu ya kifo.

### Mauaji yanayofanywa na mwenza dhidi ya mwenza

Mauaji yanayofanywa na mwenza dhidi ya mwenza ni athari kuu ya ukatili dhidi ya mwenza, ambao ni tatizo kubwa nchini Tanzania, hasa kwa wanawake walio katika mahusiano na ndoa. LHRC ilikusanya jumla ya matukio 50 ya mauaji yanayofanywa na mwenza dhidi ya mwenza, ambapo watu waliouawa 45 (asilimia 90) walikuwa wanawake na 5 (asilimia 10) ni wanaume. Idadi hii ya matukio ni ongezeko la matukio 17 ukilinganisha na mwaka 2022. Hali kadhalika, matukio haya 50 yaliyokusanywa mwaka 2023 yanafanya idadi ya matukio yaliyokusanywa na LHRC tangu mwaka 2019 kufikia 162. LHRC pia inaamini uwezekano wa matukio zaidi kutokea ila hayaripotiwi.

Nusu ya matukio yaliyoyokusanywa na LHRC yaliripotiwa katika Kanda ya Kaskazini, hasa katika Mkoa wa Kilimanjaro, na Kanda ya Ziwa. Asilimia 46 ya matukio yalisababishwa na wivu wa kimapenzi. Sababu nyingine ni pamoja na mwenza kutotaka kuendelea na mahusiano (hasa wanawake), migogoro ya kindoa, na migogoro ya mali.

**Mtazamo wa LHRC:** Ukatili dhidi ya mwenza na mauaji yanayofanywa na mwenza dhidi ya mwenza ni tishio kubwa kwa haki ya kuishi, haki ya afya, haki ya kuwa huru na salama, na uhuru dhidi ya ukatili. Idadi ya matukio yanayoripitiwa inaleta wasiwasi na kuna uwezekano mkubwa kwamba kuna matukio mengine mengine hayaripotiwi. Pia, LHRC imebaini kwamba matukio ya aina hii

yanatokea zaidi miongoni mwa makundi ya vijana na watu wazima.

**Wito wa LHRC:** Kuna haja ya wadau wote kuunganisha nguvu pamoja na kutengeneza mikakati ya kuwalinda wanawake dhidi ya ukatili dhidi ya mwenza na/au ukatili majumbani, kwa kuwa ndiyo wamekuwa waathirika zaidi. Sehemu nzuri ya kuanzia ni utungaji wa sheria ya ukatili wa kijinsia au ukatili majumbani ili kuwalinda wenza, kwa kuwa imeshafahamika kwamba matukio mengi ya ukatili wa kijinsia hutokea nyumbani.

## Upoteaji wa watu


Kwa mwaka 2023, bado hakukuwa na taarifa zozote mpya zilizotolewa kuhusu upoteaji wa watu mbalimbali katika kipindi cha miaka saba iliyopita, ikiwemo mwandishi wa habari Azory Gwanda, ambaye alipotea katika mazingira ya kutatanisha mkoani Pwani mwezi Novemba 2017.

**Wito wa LHRC:** Serikali na Jeshi la Polisi Tanzania kuongeza kasi ya upelelezi wa matukio ya watu kupotea na kutoa mrejesho wa mara kwa mara kwa umma na wanafamilia, sambamba na kuwakamata watuhumiwa. Utoaji wa mrejesho ni muhimu pia kwa familia ili ziweze kujua nini kiliwapata ndugu zao na kuendelea na maisha yao.

### Ajali za barabarani

Ajali za barabarani zinakuwa suala la haki za binadamu pale ambapo kuna uzembe umpetokea, mathalani kwenye uendeshaji wa vyombo vya usafiri au ubora wa barabara. Tathmini ya Jeshi la Polisi inaonyesha kwamba zaidi ya theluthi mbili za ajali za barabarani zinatokea kwa sababu ya makosa ya kibinadamu. Pamoja na hatua zilizopigwa katika kupunguza ajali za barabarani, zaidi ya watu 500 wanapoteza maisha kila mwaka kwa sababu ya ajali za barabarani, nyingi zikisababishwa makosa ya kibinadamu (uzembe) kama vile kuendesha vibaya, kuendesha huku mtu kalewa, kuendesha vyombo vya usafiri vyenye kasoro au vibovu, na kuvipita vyombo vingine vya moto bila umakini. Ajali za aina hii siyo tu huathiri haki ya kuishi, bali pia haki nyingine za msingi, ikiwemo haki ya kufanya kazi, haki ya afya, haki ya kuishi katika hali inayofaa, na haki ya familia.

Takwimu zinaonyesha kwamba ajali za barabarani zilipungua kutoka 1,731 mwaka 2021/22 hadi 1,283 katika kipindi cha mwezi Julai 2022 hadi Mei 2023, sawa na punguzo la asilimia 25.9. Idadi ya vifo pia ilipungua kwa asilimia 11, kutoka 946 mwaka 2021/22 hadi 842 mwaka 2022/23.




***# Ajali za barabarani na vifo nchini Tanzania, 2021/22 & 2022/23***

**Mtazamo wa LHRC:** Pamoja na jitihada mbalimbali zilizofanywa na Jeshi la Polisi, bado ajali za barabarani ni changamoto kubwa nchini Tanzania. Maisha mengi yamepotea sababu ya ajali hizo, na watu wengi kuachwa wakiwa na majeraha na ulemavu wa kudumu, jambo ambalo lina athari kubwa kwenye maendeleo ya kijamii na kitaifa. LHRC imebaini pia kwamba ukosefu wa usingizi wa kutosha kwa madereva wa mabasi ya mkoani na malori pia kunachangia ajali za barabarani, kwa sababu ya kupewa kazi nyingi na muda mchache, hivyo kukosa muda wa kupumzika, hali inayowafanya wakose umakini barabarani.

**Wito wa LHRC:** Jeshi la Polisi na wadau wengine, wakiwemo wakala wa barabara, kuongeza jitihada za kuhakikisha usalama barabarani na kuzuia ajali za barabarani, ikiwemo kupitia programu za kueneza uelewa, pamoja na kupambana na rushwa katika sekta ndogo ya usafirishaji wa kutumia barabara. Jambo lingine la muhimu ni mamlaka kuhakikisha utekelezaji madhubuti wa sheria za matumizi ya barabara na usalama barabarani, ili kuzuia na kupunguza zaidi ajali za barabarani nchini.

## 2.2. Uhuru wa Kujieleza

Kwa mwaka 2022, masuala makuu yaliyoathiri uhuru wa kujieleza kwa upande wa Tanzania Bara ni pamoja na marekebisho kiasi ya ya Sheria na Huduma za Habari ya mwaka 2016 na mashambulizi ya waandishi wa habari.

Marekebisho chanya katika Sheria ya Huduma za Habari yaliyofanyika mwaka 2023 ni pamoja na:

- Kupunguza adhabu za kukiuka vifungu vya sheria, kwa pande zote mbili za faini na vifungo; na
- Kupunguza mamlaka ya Mkurugenzi wa Kitengo cha Habari Maelezo katika kuratibu utoaji wa matangazo ya serikali, ili kuongeza uwezekano wa vyombo vya habari binafsi kupata matangazo hayo na kuongeza kipato.

Pamoja na wadau kuyapokea marekebisho ya Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016, walionyesha wasiwasi wao kutokana na urekebishaji wa vifungu vichache pekee

**31%**

Asilimia ya vifungu ambavyo Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki ilisema virekebishwe katika Sheria ya Huduma za Habari ambavyo vilirekebishwa mwaka 2023.

katika sheria hiyo, kinyume na hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki mwaka 2019. Hali kadhalika, sheria nyingine zenye vifungu vinavyominya uhuru wa kujieleza, kama vile Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015 na Kanuni za Maudhui ya Mtandao za mwaka 2020, ziliendelea kutumika mwaka 2023, hivyo kuathiri uhuru wa kujieleza mtandaoni.

Sheria zenye vifungu vinavyominya uhuru wa kuijeleza pia zinaathiri upatikanaji wa tarifa. Upatikanaji hafifu wa taarifa unaathiri zaidi makundi maalum, ikiwemo wanawake, hivyo kuwa vigumu kusikia kuhusu fursa mbalimbali na kufanya maamuzi sahihi. Upatikanaji wa taarifa pia ni muhimu katika uwezeshaji wa wanawake na makundi mengine.

Pamoja na waandishi wa habari kufurahia kuimarika kiasi kwa hali uhuru wa vyombo vya habari chini ya utawala wa Rais Samia Suluhu Hassan, wameendelea 'kusisitiza kwamba uhuru wa kweli wa vyombo hivyo hauwezi kuhakikishwa na kulindwa ipasavyo hadi pale marekebisho ya sheria yatakapofanywa.' Matukio machache zaidi ya mashambulizi au unyanyasaji wa waandishi wa habari yameripotiwa katika kipindi cha miaka ya karibuni. Kwa mwaka 2023, LHRC ilikusanya matukio mawili ya mashambulizi ya waandishi wa habari, yaliyoripotiwa katika Mikoa ya Dar es Salaam na Arusha.

Changamoto mbalimbali katika sekta ya habari, hasa mianya katika sheria, zilichangia Tanzania kushuka kwa nafasi 20 katika Viwango vya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani vya mwaka 2023. Tanzania ilishuka kutoka nafasi ya 123 mwaka 2022 hadi nafasi ya 143 mwaka 2023. Sababu kubwa iliyotajwa ni kushindwa kuchukua hatua madhubuti kurekebisha sheria zote zenye vifungu vinavyominya uhuru wa vyombo vya habari, kulingana na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu.

**Wito wa LHRC:** Serikali na Bunge kuchukua hatua na kurekebisha vifungu vilivyobakia katika sheria zote za uhuru wa kujieleza ambavyo vinaminya uhuru huo kulingana na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu.

## 2.3.Uhuru wa Kukusanyika na Uhuru wa Kujumuika

Masuala makuu yaliyoathiri ufurahiaji wa uhuru wa kukusanyika na uhuru wa kujumuika mwaka 2023 ni pamoja na Serikali kuondoa katazo la mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa na ukiukwaji wa haki ya kufanya mikutano katika baadhi ya maeneo. Wadau mbalimbali walipongeza hatua ya Serikali kuondoa katazo la mikutano lakini waliitaka kuchukua hatua madhubuti kulinda uhuru wa kukusanyika na uhuru wa kujumuika kwa kufanya marekebisho ya sheria, ikiwemo Sheria ya Vyama vya Siasa na Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi (Sura ya 322).
Kwa mwaka 2023, LHRC ilikusanya malalamiko na matukio matatu ya ukiukwaji wa uhuru wa kukusanyika na uhuru wa kujumuika, ikiwemo kuzuiwa kufanya mkutano wa hadhara.

**Mtazamo wa LHRC:** Kwa mika mingi, LHRC na wadau wengine wamekuwa wakitoa rai ya sheria zinazohusiana na uhuru wa kukusanyika na uhuru wa kujumuika kupitiwa upya na kufanyiwa marekebisho ili ziendane na Katiba na sheria za kikanda na kimataifa za haki za binadamu. Hata hivyo, ukiacha marekebisho machache yaliyofanywa katika Sheria ya Vyama vya Siasa mwaka 2023, bado vifungu vingi vinavyominya haki hizi mbili za msingi vimeendelea kuwa sehemu ya sheria hizo.

**Wito wa LHRC:** Serikali kuchukua hatua kufanya mapitio na marekebisho ya sheria zinazohusu uhuru wa kukusanyika na uhuru wa kujumuika za Sheria ya Vyama vya Siasa, Sheria ya Utekelezaji wa Haki na Wajibu wa Msingi (BRADEA), na Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali, kuondoa vifungu vyenye utata ili ziendane na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

## 2.4.Haki za Usawa mbele ya Sheria na Nafuu ya Kisheria

Masuala makuu yaliyoathiri haki ya usawa mbele ya sheria na haki ya nafuu ya kisheria mwaka 2023 kwa upande wa Tanzania Bara ni pamoja na hatua zilizochukuliwa na serikali kuimarisha upatikanaji na ufikiaji haki; vikwazo vya upatikanaji haki; changamoto katika mfumo wa haki jinai, ikiwemo ukiukwaji wa haki za mtuhumiwa mahakamani; na haki kwa watoto.


### Hatua zilizochukuliwa na Serikali kuimarisha upatikanaji haki

Kwa mwaka 2023, Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria na Mhimili wa Mahakama, ilichukua hatua mbalimbali kuimarisha upatikanaji haki, ikiwemo kupanua wigo wa utoaji wa huduma mbalimbali za kimahakama; utoaji wa msaada wa kisheria; ujengaji na

ukarabati wa majengo ya mahakama; na kutafsiri sheria mbalimbali katika Lugha ya Kiswahili ili ziweze kueleweka na wananchi wengi. Mojawapo ya matukio makubwa ilikuwa ni utambulisho na utekelezaji wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, iliyoratibiwa na Wizara ya Sheria na Katiba.

### Vikwazo vya upatikanaji haki

Wanajamii waliofikiwa na LHRC mwaka 2023 walitaja rushwa kama kikwazo kikubwa zaidi cha upatikanaji haki (asilimia 78), ikifuatiwa na kesi/shauri kuchukua muda mrefu (asilimia 49), uelewa mdogo kuhusu sheria (asilimia 48), na gharama za uwakilishi wa kisheria (asilimia 39). Uelewa mdogo kuhusu sheria na haki ulielezewa kuwa changamoto na wadau mbalimbali katika jamii katika mikoa yote iliyotembelewa.




*%Vikwazo vya upatikanaji na ufikiaji haki*

*'Rushwa ndio adui mkubwa na ndio kitu kikubwa hapa Moshi kinachokwamisha haki isipatikane, hakuna chengine.'*

***Msaidizi wa kisheria - Moshi, Kilimanjaro***

Wasaidizi wa kisheria wanafanya kazi kubwa kutoa msaada wa kisheria katika jamii. Wanajamii wengi waliofikiwa na LHRC mwaka 2023 walionyesha kuridhika na huduma za kisheria zinazotolewa na wasaidizi wa kisheria. Karibia theluthi mbili (asilimia 61) ya wanajamii walisema wanaridishwa sana (asilimia 20) na kuridhishwa (asilimia 41) na huduma hizo. Hata hivyo, changamoto za kifedha kwa wasadizi wa kisheria zinaathiri kwa kiasi kikubwa utoaji wa huduma za msaada wa kisheria.

*'Paralegals wamesaidia kwa kiasi kikubwa katika kufikisha huduma za kisheria kwa jamii.'*

***Ofisa sheria - Morogoro***

### Changamoto za haki jinai

Katika miaka ha hivi karibuni, rai mbalimbali za kuboresha mfumo wa haki jinai nchini Tanzania zimetolewa na wadau mbalimbali, ikiwemo Mh. Rais Samia Suluhu Hassan. Hii ilipeleka Mh. Rais kuunda tume ya watu 12 mnamo Mwezi Julai 2022, wakiongozwa na Jaji Mkuu Mstaafu, Mh. Mohamed Othman

Chande, kwa ajili ya kufanya uchunguzi kuhusu taasisi na mfumo wa haki jinai na kupendekeza maboresho. Mwezi Julai 2023 tume hiyo ilitoa ripoti yake, ikionyesha matokeo ya uchunguzi na kutoa mapendekezo mbalimbali ya kuboresha mfumo wa haki jinai nchini.

> Tume imebaini kuwa yapo matatizo na changamoto nyingi katika mnyororo wa Haki Jinai, tangu kwenye kuzuia uhalifu; kubaini uhalifu unapotendeka na taarifa kutolewa Polisi; uchunguzi na namna ukamataji wa watuhumiwa unavyofanyika; mashtaka yanapoandaliwa; shauri linapoendeshwa na hukumu kutolewa mahakamani; waliohukumiwa wanapokwenda kufungwa magerezani; na maisha ya wafungwa waliomaliza vifungo vyao wanaporejea uraiani.
>
> ***- Ripoti ya Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai Nchini, ukarasa wa 1***

- Kwa mujibu wa tume, taasisi za haki jinai zenye mamlaka ya ukamataji zililalamikiwa na wadau wengi katika jamii mara nyingi kutumia nguvu kubwa kupita kiasi katika ukamataji wa watuhumiwa na kuwasababishia mateso.
- Ripoti ya tume pia inaonesha kwamba uwepo wa taasisi nyingi zenye mamlaka ya kukamata pia ulilalamikiwa na wananchi, ambao walidai inakuwa vigumu kutambua taasisi iliyomkamata ndugu yao na mahali alipohifadhiwa.


**Mtazamo wa LHRC:** Tume ya Rais ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai Nchini imefanya kazi kubwa na nzuri ya kutathmini changamoto kuu katika mfumo wa haki jinai na kutoa mapendekezo.

**Wito wa LHRC:** Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Mambo ya Ndani, na taasisi za haki jinai, kuchukua hatua madhubuti kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Rais katika ripoti yake, na pia kufikiria kutelekeza mapendekezo mengine yaliyotolewa na wadau mbalimbali wakati wa ukusanyaji maoni ambayo hayajachukuliwa na tume hiyo.

### Mtazamo wa wanajamii kuhusu changamoto za haki jinai

Rushwa iliendelea kutajwa kama tatizo kubwa zaidi miongoni mwa changamoto za haki jinai (asilimia 62), ikifuatiwa na ucheleweshaji katika uchunguzi (asilimia 43), uahirishaji wa kesi mara kwa mara (asilimia 41), ucheleweshaji katika usikilizaji wa kesi

(asilimia 39), na uwekaji kuzuizini kwa muda mrefu (asilimia 35).




*% **Majibu ya wanajamii kuhusu ukubwa wa changamoto mbalimbali za haki jinai***

*'Ndugu yangu yupo mahabusu huu mwezi wa tatu sasa sababu kubwa ni upelelezi haujakamilika sasa sijui nini cha kufanya ili kupata haki ya ndugu yangu.'*

***Mwanajamii – Tanga Mjini, Tanga***

Changamoto nyingine katika mfumo wa haki jinai nchini ni pamoja na kutokuwepo kwa taasisi mahsusi ya kusimamia na kuratibu ulinzi na usalama wa watoa taarifa na mashahidi; uwepo wa vyombo vya Haki Jinai vinavyotekeleza majukumu yake kwa taswira ya kijeshi; kutokuwepo kwa upelelezi binafsi; kutokuwepo kwa ulinzi wa kutosha kwa watuhumiwa wakati wa kuingia kwenye makubaliano ya kukiri kosa; utesaji wa watuhumiwa wakati wapo chini ya ulinzi wa vyombo vya dola; utegemezi mkubwa katika kukiri kosa wakati wa upelelezi; unyimaji wa dhamana kwa makosa yaliyo na dhamana; na watuhumiwa kutofikishwa mahakamani haraka iwezekanavyo kwa mujibu wa sheria.

*'Nilitaka kumtoa mume wangu polisi kwa dhamana. Licha ya kujaribu kumpa pesa kama wanavyotaka akakataa akaniambia jiongeze sitaki pesa.Nilichokifanya nikamwambia sawa nikampa namba ili tu mume wangu atoke ndani na nilifanikiwa kumtoa ndani.'*

***Mwanajamii – Manispaa ya Kigoma, Kigoma***

## Haki kwa watoto

Mojawapo ya changamoto kuu katika usimamizi wa haki kwa watoto nchini Tanzania ni kuwachanganya watoto wanaokinzana na sheria na watu wazima katika mahabusu na magerezani. Mwaka 2023, LHRC iltembelea baadhi ya magereza nchini kwa ajili ya kutoa msaada wa kisheria na kukuta watoto wanaokinzana na sheria wamechanganywa na watu wazima. Changamoto nyingine ni pamoaja na upungufu wa mahabusu za watoto, shule za urekebishaji tabia, na mahakama za watoto; pamoja na kutotolewa kwa msaada wa kutosha kwa Maofisa wa Ustawi wa Jamii, ambao wanafanya kazi kubwa katika usimamizi wa utoaji haki kwa watoto. Pia, kuna changamoto ya upungufu wa maofisa hao wa ustawi wa jamii.

Kwa mujibu wa Tume ya Marekebisho ya Sheria Tanzania (LRCT), kuwachanganya

watoto na watu wazima mahabusu na magerezani kunahatarisha usalama wa watoto hao na kuwaweka katika hatari ya kujifunza uhalifu zaidi na kuwa wahalifu sugu. Kama ilivyopendekezwa na Tume ya Rais ya Maboresho ya Taasisi za Haki Jinai mwaka 2023, kuna haja ya kujenga mahabusu zaidi za watoto na shule za kurekebisha tabia ili kutowachanganya watoto wanaokinzana na sheria na watu wazima.

**Mtazamo na Wito wa LHRC:** Kuna haja ya kupitia na kurekebisha sheria zinazohusu haki kwa watoto, ikiwemo Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009. Hatua nyingine zilizopendekezwa na Tume ya Marekebisho ya Sheria pia zichuliwe ili kuboresha mfumo wa haki kwa watoto.

## 2.5.Haki ya kuwa Huru na Salama

Masuala makuu yaliyoathiri haki ya kuwa huru na salama Tanzania Bara mwaka 2023 ni pamoja na ukamataji na uwekaji kizuizini kinyume na sheria; unyimaji wa dhamana; ubambikaji wa kesi; na usafirishaji haramu wa binadamu.

### Kuongezeka kwa matukio ya uhalifu kunavyotishia usalama na ulinzi

Kwa mujibu wa Jeshi la Polisi, matukio makubwa ya uhalifu yaliongezeka kutoka matukio 43,771 katika kipindi cha Julai 2021 hadi Mei 2022 mpaka matukio 45,455 katika kipindi cha Julai 2022 hadi Mei 2023. Sababu za kuongezeka kwa matukio hayo ni pamoja na wananchi kujichukulia sheria mkononi, wivu wa kimapenzi, imani za kishirikina, na migogoro ya ardhi na urithi. Miongoni mwa matukio hayo yaliyotishia haki ya kuwa salama ni pamoja na mauaji ya kikatili na vitendo vya ukatili, ikiwemo ukatili wa kijinsia.

### Usalama mtandaoni

Kukosekana kwa usalama mtandaoni pia kulikuwa tishio kwa haki ya kuwa salama mwaka 2023. Wanawake na watoto, hasa katika maeneo ya mjini, walisemekana na kuonekana kuwa katika hatari zaidi ya kushambuliwa mtandaoni.

### Ukamataji na uwekaji kizuizini kinyume na sheria

Kwa mwaka 2023, LHRC ilikusanya matukio 51 ya ukamataji na uwekaji kizuizini kinyume na sheria, ambayo ni matukio 39 zaidi ya yale yaliyoripotiwa mwaka 2022. Matukio mengi yaliripotiwa katika Wilaya ya Ngorongoro. Hali kadhalika, LHRC ilikusanya matukio tisa ya ubambibakaji wa kesi, na kuna uwezekano mkubwa yapo mengine mengi ambayo hayajaripotiwa.

*'Tumegundua kwamba watuhumiwa wengi wanawekwa kizuizini kwa muda mrefu katika mahabusu za polisi bila kufikishwa mahakamani, suala ambalo ni kinyume na sheria.'*

***Jaji Mkuu Mstaafu, Mohamed Othman Chande – Mwenyekiti wa Tume ya Maboresho ya Mfumo wa Haki Jinai – Julai 2023***

## Unyimaji wa dhamana

Malalamiko ya watuhumiwa kunyimwa dhamana yaliripotiwa katika sehemu mbalimbali mwaka 2023. LHRC ikusanya matukio 21 ya unyimaji wa dhamana, yote yakihusiana na dhamana inayotolewa polisi. Matukio hayo yameongezeka kutoka matukio 18 mwaka 2022.

Mwaka 2023 pia ulishuhudia kuendelea kwa mjadala kuhusu utoaji wa dhamana kwa makosa yasiyo na dhamana na mamlaka ya utoaji wa dhamana kwa makosa hayo. Tume ya Rais ya Maboresho ya Haki Kijanai ilipendekeza marekebisho ya Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa (Sura ya 200) na Sheria ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai (Sura ya 20) ili kuipa mamlaka ya kutoa au kutotoa dhamana. Tume pia ilipendekeza kutungwa kwa sheria mahsusi ya dhamana iitwayo Sheria ya Dhamana.

Hali kadhalika, mwaka 2023 ulishuhudia utoaji wa hukumu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, ambayo ilifunguliwa na LHRC kwa kushirikiana na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), wakipinga kifungu cha 148(5) ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (Sura ya 20). Mahakama ilisema kwamba, kwa kumnyima mtuhumiwa haki zake kama vile haki ya kuchukuliwa asiye na hatia, kifungu hicho kinakiuka Ibara mbalimbali za Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu.

**Maoni na Wito wa LHRC:** LHRC inasisitiza umuhimu wa makosa yote ya jinai kuweza kutolewa dhamana, isipokuwa suala la dhamana kutolewa au la liamuliwe na Mahakama Kuu kulingana na mazingira ya kila kesi. Kumnyima mtuhumiwa dhamana moja kwa moja katika sheria kunakwenda kinyume na misingi na viwango vya haki za binadamu.

## Usafirishaji haramu wa binadamu

Usafirishaji haramu wa binadamu uliendelea kuwa tishio kwenye haki ya kuwa huru na salama pamoja na haki nyingine za msingi za haki za binadamu. LHRC ilikusanya matukio 15 ya usafirishaji haramu wa binadamu, ambayo ni matukio matatu zaidi ya yale yaliyokusanywa mwaka 2022, huku manusura wengi wakiwa ni watoto. Mnamo mwezi Mei mwaka 2023, Waziri wa Mambo ya Ndani

alisema Bungeni kwamba katika kipindi cha mwezi Julai 2022 hadi Mei 2023, jumla ya manusura 190 wa usafirishaji haramu wa binadamu waliokolewa na wizara hiyo kwa kushirikiana na wadau wengine. Manusura wengi, 184, walikuwa ni Watanzania.

**Wito wa LHRC:** Serikali, kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani, kushirikiana na wadau wengine kuimarisha hatua jitihada za kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu. Pia, bado kuna haja ya kuendelea kueneza uelewa zaidi kuhusu usafirishaji haramu wa haki za binadamu.

## 2.6.Haki ya Kushiriki katika Utawala

Masuala makuu yaliyoathiri haki ya kushiriki katika utawala kwa mwaka 2023 ni pamoja na mianya katika sheria zinazolinda haki hiyo, marekebisho ya sheria za uchaguzi na vyama vya siasa, na hukumu za mahakama kuhusu wabunge kupita bila kupingwa. Bado mianya mbalimbali katika Katiba na sheria nyingine kama vile Sheria ya Vyama vya Siasa na Sheria ya Taifa ya Uchaguzi hazijarekebishwa kuelekea chaguzi za mwaka 2024 na 2025. Mnamo mwezi Novemba mwaka 2023, miswada mitatu ya sheria za uchaguzi na vyama vya siasa, ambayo ni Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge, na Serikali za Mitaa; Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Masuala ya Vyama vya Sisasa; na Mswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Hata hivyo, uchambuzi uliofanywa na wadau mbalimbali, ikiwemo LHRC, umeonyesha kwamba marekebisho yaliyopendekezwa katika Sheria ya Vyama vya Siasa hayatoshelezi na yatabadilisha sheria kwa kiasi kidogo. Mianya iliyoonekana katika muswada wa sheria hiyo ni pamoja na kutochukua mapendekezo mengi muhimu yaliyotolewa na Kikosi Kazi cha Rais cha Demokrasia ya Vyama Vingi kilichoundwa na Mh. Rais na kutoa ripoti yake mwaka 2022.

Mnamo mwezi Machi mwaka 2023, Mahakama Kuu ya Tanzania ilitoa hukumu yake katika kesi inayohusu vifungu kadhaa katika Sheria ya Uchaguzi na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa vinavyoruhusu wagombea wa nafasi za ubunge na udiwani kupita bila kupingwa. Mahakama ilisema kwamba vifungu hivyo vinaenda kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, hususan Ibara ndogo za (1) na (2) za Ibra ya 21.

### Elimu ya Uraia na Mpiga Kura

Wakati nchi ikielekea katika chaguzi za mwaka 2024 na 2025, suala jingine la muhimu kwa upande wa ushiriki katika utawala ni elimu ya uraia na mpiga kura. LHRC inatoa rai kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuhakikisha elimu hii inatolewa kwa wanajamiii mapema iwezekanavyo. Hii itasaidia makundi mbalimbali katika jamii kama vile wanaume, wanawake, vijana, wazee, na watu wenye ulemavu, kuelewa haki zao, mfumo wa kisiasa, na mzunguko wa uchaguzi, kama ambavyo masuala haya yameainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na sheria nyingine zinazohusu uchaguzi, pamoja na mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa ya haki za binadamu. Ni muhimu pia makundi haya yakaelewa mchakato mzima wa upigaji kura. Elimu inayotolewa pia izingatie mahitaji ya kijinsia na kutolewa katika majukwaa mbalimbali ili kuhakikisha watu wote wanapata taarifa sahihi kuhusu uchaguzi na kwa wakati. Asasi za kiraia zina nafasi kubwa katika utoaji wa elimu hii ya uraia na mpiga kura, hivyo zihakikishe zinapata vibali mapema na kuanza kutoa elimu hizo kabla ya chaguzi.

## 2.7.Uhuru dhidi ya Utesaji na Kutendwa kama siyo Binadamu

Kwa mwaka 2023, matukio na malalamiko kuhusu utesaji yaliripotiwa katika sehemu mbalimbali za Tanzania Bara, ambapo LHRC ilikusanya matukio 57, yakiongezeka kutoka 44 mwaka 2022. Matukio haya yalijumuisha utesaji wa watoto na utesaji wa watuhumiwa waliokuwa chini ya ulinzi au mikononi mwa maofisa wa dola.

## 2.8.Uhuru dhidi ya Ukatili

Baadhi ya wanawake, watoto, wanaume, watu wenye ulemavu, na wazee walifanyiwa vitendo mbalimbali vya ukatili wa kimwili, kingono, kiuchumi, na kisaikolojia mwaka 2023. Manusura wengi wa ukatili walikuwa ni watoto, wakifuatiwa na wanawake.

LHRC ilikusanya matukio 27 ya ukatili dhidi ya wanaume, yakiongezeka kutoka matukio 9 mwaka 2022. Miongoni mwa matukio hayo, kumi na mbili yaliripotiwa mkoani Rukwa na saba mkoani Kilimanjaro. Mojawapo ya changamoto ya mapambano dhidi ya aina hii ya ukatili ni wanaume wengi kutokuwa na mwamko wa kuripoti matukio ya ukatili wanayofanyiwa sababu ya aibu.

.



***Mwanaume mwenye ulemavu akionyesha makovu yaliyotokana na kushambuliwa na mke wake jijini Dodoma mwaka 2023***

Takwimu za Jeshi la Polisi zinaonyesha kwamba jumla ya matukio 35,013 ya ukatili dhidi ya wanaume yaliripotiwa katika kipindi cha mwaka 2019 hadi 2021, sawa na wastani wa matukio 11,671 kila mwaka na 973 kila mwezi. Matokeo ya utafiti kuhusu demografia na afya uliofanyika mwaka 2022 yanayonyesha kwamba asilmia 2 ya wanawake wenye umri wa miaka 15 hadi 49 ambao wamewahi kuolewa au kuwa na mwenza walianza kuwafanyia vitendo vya ukatili wa kimwili wenza wao kabla hata ya wao kuanza kufanyiwa vitendo hivyo. Njombe (asilimia 7) ndiyo ilikuwa na asilimia kubwa zaidi ya wanawake walioanzisha vitendo hivyo vya ukatili wa kimwili dhidi ya wenza wao.

## 2.9. Haki ya Faragha

Mwaka 2022, sheria muhimu ya ulinzi wa taarifa binafsi ilitungwa ili kulinda haki ya faragha. Hata hivyo, kuna marekebisho kadhaa yanahitajika katika sheria hiyo ili iendane na viwango vya kimatainfa vya haki za binadamu. Kwa mwaka 2023, katazo la matumizi ya mtandao wa kibinafsi wa kidijitali (VPN) bila ya kuwa na kibali kutoka kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), lililotolewa mwezi Oktoba 2023, liligusa ulinzi wa haki ya faragha. Wadau mbalimbali, ikiwemo LHRC, walionyesha wasiwasi wa katazo hilo kuingilia haki ya faragha na kuathiri haki nyingine za kidijitali na binadamu.



03

Sura ya Tatu

# HAKI ZA KIUCHUMI, KIJAMII, NA KIUTAMADUNI

SURA YA TATU:
# HAKI ZA KIUCHUMI,KIJAMII, NA KIUTAMADUNI

Masuala makuu yaliyoathiri ufurahiaji wa haki za kiuchumi, kijamii, na kiutamaduni mwaka 2023 ni pamoja na ufinyu wa bajeti; mazingira duni ya kazi; ukosefu wa ajira; upungufu wa wafanyakazi; upungufu wa vifaa, nyenzo, na majengo; ukiukwaji wa haki za wafanyakazi; na aina tofauti za ukatili, hasa dhidi ya watoto, wanawake, na watu wenye ulemavu.


## 3.1. Haki ya Elimu

### Hatua zilizochukuliwa na Serikali

Serikali iliendelea kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha utekelezaji endelevu wa haki ya elimu, ikiwemo kupitia utekelezaji wa sera ya elimu bila malipo ya ada. Hali kadhalika, mwaka 2023 Serikali ilikamilisha mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014. Hata hivyo, changamoto mbalimbali ziliendelea kuikumba sekta ya elimu, ikiwemo ufinyu wa bajeti na upungufu wa walimu, nyumba za walimu, madarasa, na matundu ya vyoo.

### Ufinyu wa bajeti

Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya sekta ya elimu kwa mwaka wa fedha 2023/24 iliongezeka kiasi ukilinganisha na mwaka wa fedha wa 2022/23. Hata hivyo, bajeti hiyo bado haikidhi kiwango cha kimataifa kuhusu bajeti ya elimu, ambacho ni asilimia 20 ya bajeti ya nchi kutengwa kwa ajili ya elimu. Hali kadhalika bajeti ambayo imekuwa ikitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa elimu bila ada pia imekuwa haijitoshelezi. Changamoto hizi za kibajeti ziliendelea kuathiri ubora wa elimu mwaka 2023.





***Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya sekta ya elimu kwa miaka ya fedha fedha 2018/19 hadi 2023/24 na asilimia yake katika bajeti ya taifa.***

Wadau wa elimu waliendelea kukosoa bajeti iliyotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa sera ya elimu bila ada, wakidai kwamba kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya wanafunzi wa shule za msingi (Sh. 10,000) na sekondari (Sh. 25,000) hakikidhi mahitaji yao katika taasisi za elimu.

**Wito na Rai ya LHRC:** Ili kuboresha ubora wa elimu nchini, Serikali haina budi kuongeza uwekezaji katika sekta ya elimu, ikiwemo kwa upande wa miundombinu, na kuhakikisha walau asilimia 20 ya bajeti ya taifa inaenda kwenye elimu.

## Mtazamo wa wanajamii kuhusu changamoto za kielimu

Wanajamii mbalimbali waliofikiwa na LHRC kupitia utafiti wa haki za binadamu mwaka 2023 waliainisha changamoto mbalimbali katika elimu, huku upungufu wa walimu ukitajwa kama changamoto kuu zaidi (asilimia 46), ikifuatiwa na changamoto za ushirikiano duni kutoka kwa wazazi (asilimia 43), mimba za utotoni (asilimia 42), na upungufu wa madarasa (asilimia 41).




***% Majibu kuhusiana na mtazamo wa jamii kuhusu masuala makuu yanayoathiri ufurahiaji wa haki ya elimu***

Upungufu wa walimu ni changamoto zaidi katika shule za msingi ukilinganisha na sekondari, na hii imechangiwa zaidi na kuongezeka kwa uandikishaji wa wanafunzi wapya kunakotokana na utekelezaji wa sera ya elimu bila ada. Upungufu wa walimu wa elimu maalum pia ni changamoto kwa upande wa utoaji wa elimu jumuishi.
Changamoto nyingine kuu zilizotajwa na walau theluthi moja (asilimia 33) hadi asilimia 35 ya wanajamii ni pamoja na upungufu wa vyoo/matundu ya vyoo; umbali wa shule; vitendo vya ukatili dhidi ya watoto; ajira kwa watoto; na ndoa za utotoni. Changamoto hizi zilichangia wanafunzi kuacha shule, jambo ambalo ni tatizo nchini, hasa katika Mikoa ya Geita, Mwaza, Tabora, Kagera, Simiyu, na

Dodoma. Wasichana na wavulana waliacha shule kwa sababu mbalimbali, ikiwemo kuolewa na kwenda kufanya kazi.

*'Watoto wengi wa kike wanaacha shule wanaenda kuolewa wakiwa bado na umri mdogo, na kwa upande wa watoto wa kiume wanaacha shule na kwenda kujihusisha na shughuli za kilimo, na kuchunga mifugo hasa maeneo ya vijijini.'*

***Msaidizi wa kisheria – Tabora***

## Ushirikiano duni kutoka kwa wazazi

Karibia theluthi mbili (asilimia 62) ya wajamii waliohojiwa walisema kwamba wamewahi kushuhudia au kusikia matukio ya wazazi kuwaambia watoto wao wafeli mitihani yao ya taifa makusudi. Matukio hayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Pwani, Njombe, Mbeya, Dodoma, Mtwara, na Tabora. Sababu zilizotolewa ni pamoja na ndoa za utotoni, matokeo mabaya ya mitihani ya taifa katika baadhi ya shule, wazazi kutokuwa na elimu au mwamko wa elimu, wazazi kuona kama wanapoteza pesa zao kuwasomesha watoto, na wazazi kuepuka gharama za kusomesha watoto mara baada ya kufaulu mitihani yao ya taifa.

*'Ni kweli kuna wazazi wanawashawishi watoto wao wafeli mitihani yao kwa sababu mbalimbali, ikiwemo kuolewa na kufanya kazi, wakisema hawana hela za kusomesha.'*

***Msaidizi wa kisheria – Mtwara***

## Usafi wa hedhi

Changamoto za usafi wa hedhi ziliendelea kuathiri ufurahiaji na utekelezaji wa haki ya elimu kwa upande wa wasichana, ikichangiwa na ukosefu wa taulo za kike, upatikanaji hafifu wa maji safi na salama, vyoo vichafu, na ukosefu wa vyumba vya kubadilishia nguo. Wasichana, hasa wanaokaa maeneo ya vijijini, walionekana kuathirika zaidi na changamoto hizo.

*'Wengi wetu kipindi cha hedhi huwa hatuji shule na hata ukija shule unakuwa hauko huru kwani wengi wetu tunatumia matambara ambayo yanaweza kuloa damu na kujikuta unapata aibu mbele ya wanaume.'*

***Msichana wa kidato cha tatu – Kigoma***

## Ukatili dhidi ya watoto

Baadhi ya watoto wanaosoma shule hukumbana na vitendo mbalimbali vya ukatili wa kimwili, ikiwemo adhabu kali za viboko; ukatili wa kingono, ikiwemo unaofanywa na walimu; ukatili wa kisaikolojia, ikiwemo kwenda shule na njaa; na ukatili wa kiuchumi,

ikiwemo kuwanyima watoto wa kike elimu zaidi 'sababu wataolewa.' Watoto wanaokaa mbali na shule na kulazimika kutembea umbali mrefu wapo katika hatari zaidi ya kufanyiwa vitendo vya ukatili, hasa ukatili wa kingono.

### Ndoa na mimba za utotoni

Ndoa na mimba za utotoni viliendelea kuwa vikwazo vikubwa kwa ndoto ya wasichana kupata elimu mwaka 2023. Wasichana katika maeneo mbalimbali ya nchi waliendelea kuacha shule kwa sababu ya ndoa na mimba za utotoni. LHRC ilkusanya matukio 14 ya ndoa za utotoni, ambayo ni mawili pungufu ya yale yaliyokusanywa mwaka 2022. Pia, LHRC ilikusanya matukio 2,953 ya mimba za utotoni yaliyoripotiwa katika mikoa mbalimbali.

- Baadhi ya wazazi, hasa katika maeneo ya vijijini, wanawaambia mabinti zao wafeli au kuacha shule ili waolewe.
- Mila zenye madhara na umaskini vilitajwa kama miongoni mwa vichocheo vikubwa vya ndoa za utotoni.
- Miongoni mwa matukio yaliyokusanywa na LHRC mwaka 2023 ni pamoja na wasichana ambao siyo tu walipewa ujauzito bali pia waliambukizwa magonjrwa ya zinaa, ikiwemo UKIMWI.

### Changamoto nyingine

Changamoto nyingine za kielimu zilizoripotiwa mwaka 2023 ni pamoja na utoro, usafirishaji haramu wa watoto, mazingira magumu ya kufundishia ya walimu, na kurudi shule kwa wasichana waliopata ujauzito na walio na watoto.

- Utoro unachangia wanafunzi kuacha shule kwa asilimia 90. Utoro, hasa katika maeneo ya vijijini, unachochewa na changamoto za usafi wa hedhi, umbali wa shule, na ushirikiano duni wa wazazi.
- Mwaka 2023 wadau pia waliendelea kupendekeza marekebisho ya sheria ili kuingiza kwenye sheria za elimu vifungu kuhusu wasichana waliopata ujauzito na walio na watoto kurudi shule na kuendelea na masomo, baada ya Serikali kutoa mwongozo wa wasichana hao kurudi shule. Wadau walidai pia kwamba wasichana wengi wanaorudi au kutaka kurudi shule wanapata changamoto mbalimbali, ikiwemo kutopata msaada kutoka katika familia zao na kuhitaji msaada zaidi kutoka kwa Serikali ili kuendelea vizuri na masomo.

### Elimu kuhusu ukatili wa kijinsia na haki za binadamu katika mitaala ya elimu

Mwaka 2023 wadau mbalimbali walipendekeza kuingizwa kwa elimu kuhusu ukatili wa kijinsia na elimu kuhusu haki za

binadamu kuingizwa katika mitaala ya elimu nchini.

## 3.2. Haki ya Afya

Masuala makuu yaliyoathiri haki ya afya kwa upande wa Tanzania Bara mwaka 2023 ni pamoja na ufinyu wa bajeti; upungufu wa wafanyakazi; matatizo ya afya ya akili; upungufu wa mashine, madawa, na vifaa tiba; na changamoto katika utoaji wa huduma za afya ya mama.

### Hatua zilizochukuliwa na Serikali

Serikali iliendelea kuchukua hatua mbalimbali katika utekelezaji wa haki ya afya, ikiwemo kuajiri wafanyakazi zaidi, kununua madawa na vifaa tiba muhimu, na ujenzi wa vituo vipya vya afya na majengo mapya.

### Utengaji wa bajeti

Kwa mwaka wa fedha 2023/24, bajeti iliyotengwa kwa ajili ya sekta ya afya ilongezeka ukilinganisha na mwaka wa fedha uliopita. Hata hivyo, bajeti hiyo bado iliendelea kuwa chini ya kiwango kinachotakiwa, ambacho ni bajeti ya afya kuwa asilimia 15 ya bajeti ya taifa, kwani bajeti illiyotengwa ilikuwa ni asilimia 5.4 pekee ya bajeti ya taifa.

**Mtazamo na Wito wa LHRC:** Ili kufikia viwango vya kimatifa na malengo mbalimbali kuhusu afya, Serikali haina budi kuongeza zaidi bajeti ya sekta muhimu ya afya.

**50%** Asilimia ya upungufu wa wafanyakazi katika sekta ya afya.

### Bima ya Afya

Sheria ya bima ya afya, iliyokuwa inasubiriwa kwa muda mrefu, hatimaye ilitungwa mwaka 2023. Hatua hii ni muhimu katika kulinda haki ya afya. Kwa upande mwingine, kitita cha bima ya afya cha Toto Afya kiliondolewa katika bima, jambo ambalo lilileta wasiwasi mkubwa miongoni mwa wazazi na wadau mbalimbali wa haki afya na haki za binadamu kwa ujumla.

### Huduma za Afya ya Mama

Haki ya wanawake ya huduma bora za afya ya mama ziliendelea kuathiriwa na masuala na changamoto mbalimbali mwaka 2023. Utoaji wa huduma za afya ya mama, hasa katika hospitali na vituo vya afya vya serikali, uliendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali, ikiwemo umbali wa hospitali na vituo hivyo; upungufu wa wafanyakazi, ikiwemo wauguzi; na vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa akinamama. Changamoto hizi zilichangia katika kusababisa vifo vya akinamama vinavyotokana na ujauzito.
Kwa mwaka 2023, LHRC pia ilikusanya matukio ya wanawake wajawazito kulipishwa

huduma za afya ya mama ambazo zinatakiwa kutolewa bure kulingana na sera ya Serikali.

> Takribani vifo 80 vya akinamama vinavyotokana na ujauzito vinatokea kila mwezi.

## Upungufu wa vitanda


Matukio ya upungufu wa vitanda katika wodi za wajawazito katika maeneo mbalimbali nchini yaliripotiwa sana mwaka 2023. Jambo hili lilisababisha wanawake wajawazito kutumia vitanda pamoja. Katika baadhi ya hospitali katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani iliripotiwa kwamba wanawake wawili hadi watatu walitumia kitanda kimoja.

## Afya ya hedhi na hedhi salama

Afya ya hedhi na hedhi salama bado ni changamoto kwa wanawake na wasichana wengi nchini Tanzania, hasa maeneo ya vijijini. Upatikanaji wa taulo za kike ni changamoto kubwa. Taulo inayotumiwa zaidi na wasichana na wanawake wenye umri wa miaka 15 hadi 49 ni kipande cha nguo au tambara (asilimia 53), ikifuatiwa na taulo za kike siziso za kufua (asilimia 37). Wasichana na wanawake waishio vijijini hutumia zaidi taulo za kipande cha nguo au tambara (asilimia 63) kuliko wale waishio maeneo ya mijini (asilimia 37).

## Afya ya akili na kujitoa uhai

Afya ya akili iliendelea kuwa mojawapo ya changamoto kubwa kwa upande wa afya mwaka 2023. Matatizo ya afya ya akili yalipelekea baadhi ya watu, hasa vijana, kuamua kufanya uamuzi wa kujitoa uhai. LHRC ilikusanya matukio 57 ya watu kujitoa uhai, ambayo ni 22 zaidi ya yale iliyokusanya mwaka 2022. Asilimia 79 ya waathirika walikuwa ni wanaume na robo walikuwa ni watoto. Waathirika wengi (asilimia 46) walikuwa ni vijana wenye umri wa miaka 18 hadi 35.




***% Matukio ya watu kujiua yaliyokusanywa kiumri na LHRC***

Watu waliojitoa uhai walikuwa na fani mbalimbali, ikiwemo utumishi wa umma, uofisa wa dola, biashara, kilimo, na ualimu. Uchambuzi wa matukio yaliyoripotiwa ulionyesha kwamba waathirika hao walifikia maamuzi hayo kwa sababu mbalimbali,

ikiwemo kusababisha ajali, madeni, kutelekezwa, kukosa ada, kuigiza tukio katika filamu, ugonjwa, kupata hasara, kuachwa katika mahusiano, kuadhibiwa na mzazi, kuwa na mahusiano nje ya ndoa, wivu wa kimapenzi, kusimamishwa kazi, na ugumu wa maisha.

### 3.3. Haki ya Maji Safi na Salama

Pamoja na juhudi mbalimbali zilizofanywa kuongeza upatikanaji wa maji, bado kuna changamoto kadhaa zimeendelea kuathiri haki ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi, ikiwemo ufinyu wa bajeti; uvujaji na upotevu wa maji; maji kutopatikana kirahisi katika baadhi ya maeneo; na athari za mabadiliko ya tabianchi. Pamoja na bajeti inayotengwa kwa ajili ya sekta ya maji kuongezeka katika miaka ya fedha ya hivi karibuni, kuanzia mwaka wa fedha 2021/22, bado fedha zinazotengwa hazifikii kiwango cha chini kinachopendekezwa cha asilimia 5.5. ya bajeti, pamoja na viwango vingine. Shughuli za kibinadamu pia zimendelea kusababisha uchafuzi wa vyanzo vya maji katika maeneo mbalimbali nchini. Hali kadhalika, mabadiliko ya tabia nchi yalisababisha uchelewaji wa mvua, ukame, na mafuriko, ambavyo vilichangia kukauka kwa vyanzo vya maji, uharibifu wa miundombinu ya maji, na uwepo wa mgao wa maji.

### 3.4. Kufanya Kazi

Masuala makuu yaliyoathiri haki ya kufanya kazi mwaka 2023 ni pamoja na ukiukwaji wa haki za wafanyakazi, mazingira duni ya kazi, na uelewa mdogo kuhusu sheria za kazi na haki za wafanyakazi. LHRC ilikusanya malalamiko mapya 2,653 ya ukiukwaji wa haki za wafanyakazi, ambayo 624 (asilimia 24) yaliwahusu wanawake na 2,029 (asilimia 76) yaliwahusu wanaume. Malalamiko mengi (asilimia 54) yalihusu kufukuzwa kazi kinyume na sheria, yakifuatiwa na mafao (asilimia 29). Ukiukwaji uliokithiri wa haki za wafanyakazi uliendelea kuwa changamoto kubwa nchini Tanzania.

Hali kadhalika, malalamiko kuhusu ukiukwaji wa haki za wafanyakazi majumbani yaliripotiwa sana mwaka 2023. Ukiukwaji huo ni pamoja na kutolipwa mishahara na kulipwa mishahara chini ya kiwango cha chini kilichowekwa na Serikali. Mkoani Mwanza, baadhi ya wafanyakazi majumbani na viongozi wao kutoka mikoa sita walitoa malalamiko yao kuhusu kulipwa chini ya kiwango cha chini kwa mujibu wa Waraka mpya wa Viwango vya Chini vya Mshahara mwaka 2022, ambacho ni Shillingi 60,000.
Masuala mengine ya ukiukwaji wa haki za wafanyakazi ni pamoja na vitendo vya ukatili mahala pa kazi, ubaguzi wa watu wenye ulemavu, waajiri kutopeleka michango ya

hifadhi ya jamii kwenye mifuko husika, na ucheleweshaji wa malipo ya mishahara na mafao.

- Kwa mwaka 2023, ukatili mahala pa kazi uliendelea kuwa changamoto, hasa kwa wafanyakazi wa kike katika sekta binafsi.
- Watu wenye ulemavu waliendelea kulalamika kuhusu ubaguzi katika soko la ajira. Hali kadhalika, tabia ya baadhi ya waajiri kutowasilisha michango ya hifadhi ya jamii iliendelea kuwa mwiba kwa haki za wafanyakazi.
- Mnamo mwezi Juni 2023, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ulitangaza kwamba umefungua kesi 350 dhidi ya waajiri ambao hawajawasilisha michango ya hifadhi ya jamii katika maeneo mbalimbali nchini.
- Miongoni mwa malalamiko ya ucheleweshaji wa mishahara na mafao yaliyoripotiwa mwaka 2023 yalitolewa na walimu na wafanyakazi majumbani.

### 3.5. Kumiliki Mali

Kwa mwaka 2023, masuala makuu yaliyoathiri ufurahiaji na utekelezaji wa haki ya kumiliki mali ni pamoja na migogoro ya ardhi na unyang'anyi wa mali kutoka kwa wajane na wazee. Migogoro ya ardhi ilidaiwa kuwa changamoto kuu inayowakabili wafugaji katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara. Wafugaji walielezea wasiwasi wao mkubwa kuhusu mienendo ya ukiukwaji wa haki yao ya kumiliki mali, hususan kupitia ukamataji na upigaji mnada wa mifugo yao inayosemekana kuingia katika mbuga za wanyama na maeneo mengine ya hifadhi. Viongozi wa umoja wa wafugaji walitoa malalamiko kuhusu suala hili na kuomba marekebisho ya sheria kwa Tume ya Rais ya Kuboresha Mfumo wa Haki Jinai.

LHRC ilikusanya matukio ya migogoro ya ardhi yaliyoripotiwa katika Mikoa ya Shinyanga, Mbeya, Kigoma, Arusha, Lindi, Mwanza, Dodoma, Manyara, Singida, na Tanga. Baadhi ya migogoro hiyo ilipelekea vifo na uharibifu wa mali. Madhara makubwa zaidi yalitokea kwenye migogoro na mapigano kati ya wakulima na wafugaji.

Kupigia programu yake ya utoaji wa msaada wa kisheria katika vituo vyake vya Dar es Salaam, Arusha, na Dodoma, LHRC ilipokea jumla ya malalamiko 12,205 kuhusu ukiukwaji wa haki ya kumiliki mali (ardhi), ambapo malalamiko 4,225 (asilimia 35) yalitolewa na wanawake na matukio 7,980 (asilimia 65) yalitolewa na wanaume.

LHRC pia ilikusanya matukio 15 ya utoaji kinguvu wa nguvu wa wanawake katika mali zao. Hali kadhalika, kuliripotiwa matukio

kadhaa ya wazee kutishiwa na watoto wao na kulazimshwa kuwapatia urithi. Mila baguzi zilendelea pia kuwanyimwa wanawake na wasichana haki za kumiliki na kurithi mali.

Changamoto nyingine zinazohusiana na ardhi zilizoripotiwa mwaka 2023 ni pamoja na uelewa mdogo kuhusu sheria na haki za ardhi, ucheleweshaji katika utoaji wa fidia kufatia utwaaji wa ardhi, makazi yasiyo rasmi, na ukopaji mikopo kwa dhamana ya mali.

## 3.6. Haki ya Kuishi katika Hali Inayofaa

Masuala makuu yaliyoathiri haki ya kuishi katika hali inayofaa Tanzania Bara ni pamoja na upungufu wa chakula; upatikanaji wa chakula chenye virutubisho; uwezo wa kumudu gharama za chakula; na upatikanaji wa makazi yanayofaa.

### Upungufu wa chakula

Upungufu wa chakula uliripotiwa katika baadhi ya maeneo ya Tanzania Bara. Mathalani, watu 900,000, wakazi wa halmashauri za wilaya 21, hasa za Longido na Monduli, waliripotiwa kukabiliwa na upungufu mkubwa wa chakula. Upungufu huo ulichangiwa zaidi na kipindi kikubwa cha ukame na mvua sizizotabirika, hali iliyoathiri uzalishaji wa mazao na malisho, pamoja na upatikanaji wa maji. Mabadiliko ya tabianchi yaliathiri pia uzalishaji wa mbegu zenye ubora unaotakiwa na uzalishaji wa chakula. Hata hivyo, ilitabiriwa kwamba hali hiyo ya upungufu wa chakula ingepungua mwaka 2024.

### Bajeti ya sekta ya kilimo

Kilimo ni uti wa mgogo wa uchumi wa Tanzania na mwajiri mkuu wa wafanyakazi nchini. Hii inafanya sekta ya kilimo siyo tu kuwa muhimu kwa ajili ya uzalishaji wa chakula na utekelezaji wa haki ya chakula, bali pia katika kutegeneza ajira na kuwawezesha Watanzania wengi kujiingizia kipato, ambacho pia kunawasaidia kuweza kumudu kuishi katika makazi yanayofaa. Hata hivyo, bado bajeti inayotengwa kwa ajili ya sekta hii muhimu haijaweza kufikia kiwango cha chini kilichowekwa katika Tamko la Umoja wa Afrika la Malabo la mwaka 2014, ambacho ni asilimia kumi ya bajeti ya taifa kupelekwa katika sekta ya kilimo.

Kwa mwaka wa fedha 2023/24, bajeti iliyotengwa kwa ajili ya sekta ya kilimo, ikiwemo Mifugo na Uvuvi, ilikuwa ni Sh. Trilioni 1.47, ikiongezeka kutoka Sh. Trilioni 1.2 katika mwaka wa fedha 2022/23. Hii ni sawa na asilimia 3.3 ya bajeti ya taifa pekee, hivyo chini ya kiwango cha chini cha asilimia 10.

### Makazi na nyumba

Kuhusiana na makazi na nyumba, ilipotiwa

mwaka 2023 kwamba Tanzania inakabiliwa na upungufu wa nyumba milioni 3.8. Pia, iliripotiwa kwamba gharama za vifaa vya ujenzi zimekuwa zikipanda katika maeneo mbalimbali nchini, hivyo kufanya iwe ngumu kwa wananchi kumudu gharama hizo na kujenga nyumba zinazofaa. Hali hii imechochewa pia na mafuriko makubwa na maporomoko ya matope katika sehemu mbalimbali za nchi, ambayo yalileta athari mbalimbali, ikiwemo kuharibu nyumba na miundombinu mbalimbali.

**Mtazamo wa LHRC**: Makazi na nyumba bora vina umuhimu mkubwa katika ufurahiaji na utekelezaji wa haki nyingine za binadamu. Hata hivyo, bado watu wengi wanakabiliwa na changamoto ya kuishi katika nyumba zisizo bora, kote mijini na vijijini. Waathirka wakuu katika hili ni wanawake, watoto, na makundi mengine maalum.

**Wito wa LHRC:** Serikali, kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi, kuongeza juhudi za kuboresha makazi na kuhakikisha upatakanaji wa nyumba bora za kuishi.

### 3.7. Haki ya Hifadhi ya Jamii

Masuala makuu yaliyoathiri ufurahiaji wa haki ya hifadhi ya jamii mwaka 2023 ni pamoja na watu wengi kutokuwa wanufaika wa mifumo ya hifadhi ya jamii; bima ya afya, ikiwemo utungwaji wa sheria ya bima ya afya kwa wote; na waajiri kutowasilisha michango ya wafanyakazi kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii. Baadhi ya waajiri walituhumiwa kutowasilisha michango ya hifadhi ya jamii, kama ilivyokuwa katika miaka ya nyuma. Wazee katika mikoa 20 ya Tanzania Bara iliyotembelewa na LHRC mwaka 2023 walilamika kuhusu kutokuwepo kwa pensheni kwa wazee wote na kutokuwa na kipato cha kueleweka kama mojawapo ya changamoto kuu zinazowakabili na kuwafanya waishi maisha magumu na umaskini mkubwa. Pia, baadhi ya wazee waliostaafu walionyesha wasiwasi kuhusu utoshelezi wa mafao na ucheleweshaji na ukiritimba katika utoaji wa mafao hayo.

**Wito wa LHRC:** Serikali, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira, na Watu wenye Ulemavu), kuhakikisha utekelezaji madhubuti wa sheria za ulinzi wa kijamii na kuhakikisha waajiri wanapeleka michango ya kila mwezi kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii.



04

Sura ya Nne

# HAKI ZA KIUJUMLA

SURA YA NNE:

# HAKI ZA KIUJUMLA

Masuala makuu yaliyoathiri ufurahiaji wa haki za kiujumla ni pamoja na usimamizi mbovu, matumizi mabaya, na ubadhirifu wa fedha za umma; uchafuzi na uharibifu wa mazingira; na athari za mabadiliko ya tabianchi.

## 4.1. Haki ya Maendeleo

Ufurahiaji wa haki ya maendeleo hutegemea utekelezaji wa haki za kiraia, kisiasa, kijamii, na kiuchumi. Katika muktadha huo, ufurahiaji wa haki hii ya msingi mwaka 2023 uliathiriwa na changamoto mbalimbali zilizoainishwa katika sura nyingine zilizopita, pamoja na rushwa na usimamizi mbaya, matumizi mabaya, na ubadhirifu wa fedha za umma..

### Sakata la Mkataba wa DP World

Katika kipindi cha nyuma, Tanzania imekuwa ikiteseka na migogoro ya uwekezaji inayotokana na mikataba ya uwekezaji na nchi nyingine au kampuni toka nchi nyingine, ambapo imeshapoteza kesi za migogoro hiyo kadhaa na kulazimika kulipa fidia kubwa. Hali hii imekuwa ikiathiri kwa kiasi kikubwa ufurahiaji na utekelezaji wa haki ya maendeleo. Mwaka 2023 ulitokea mjadala mkubwa kuhusu mkataba wa uwekezaji kati ya Tanzania na kampuni ya uwekezaji kutoka Dubai iitwayo DP World. Makubaliano katika mkataba huo yalilenga kuipa kampuni hiyo mamlaka ya kuendesha sehemu ya Bandari ya Dar es Salaam. Baada ya mkataba huo kuibuliwa, wadau mbalimbali walielezea wasiwasi wao kuhusu baadhi ya vifungu katika mkataba huo kuwa na utata, huku wakionya kwamba kama vifungu hivyo havitarekebishwa au kuondolewa kabisa basi nchi itakuwa katika hatari ya kuingia hasara pale utakapotokea mgogoro katika utekelezaji wa mkataba huo na mikataba mingine itakayotokana na mkataba huo. Baadhi ya wakosoaji wa mkataba huo, wakiongozwa na Boniface Mwabukusi (Wakili) waliamua kuchukua hatua ya kufungua kesi ya kupinga mkataba huo katika Mahakama mnamo mwezi Juni 2023, huku mabishano mbalimbali kati ya wanaounga mkono mkataba kama ulivyo na wanaoukosoa na kutaka urekebishwe yakilendelea katika maeneo na majukwaa mbalimbali nchini.

**Wito wa LHRC:** Serikali iwe inawashirikisha wadau kuijadili na kuichambua mikataba mikubwa ya uwekezaji kabla ya kuingia kwenye mikataba hiyo na nchi au makampuni ya nje ya nchi ili kulinda vizuri zaidi maslahi ya taifa na kuondoa au kupunguza uwezekano wa kuingia hasara kubwa pale ambapo migogoro ya uwekezaji itatokea, kama ambavyo imekuwa katika kipindi cha nyuma.

### Viashiria vya Rushwa na Usimamizi Mbaya, Matumizi Mabaya, na Ubadhirifu wa Fedha za Umma

Suala jingine kubwa linalohusu haki ya maendeleo lilijitokeza mwaka 2023 ni matukio ya usimamizi mbaya, matumizi mabaya, na ubadhirifu wa fedha za umma yaliyoibuliwa katika Ripoti za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zilizotolewa mwaka huo, yakiashiria rushwa na udanganyifu. Wadau mbalimbali walitoa maoni kuhusu matukio hayo huku wakilalamikia kukosekana kwa uwajibikaji kwa watu na taasisi zilizotajwa kuhusuka matukio hayo.

Kwa mujibu wa tathmini iliyofanywa na Shirika la WAJIBU, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alikuta viashiria vya rushwa, udanganyifu, na ubadhirifu vyenye thamani ya Sh. Billioni 3,084.55 (matumizi yasiyo na manufaa au tija). Matumizi hayo yasiyo na tija yalipungua kwa asilimia 33 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2020/21. Asilimia 65 ya matumizi yasiyo na tija yalifanywa na taasisi za umma, na matumizi hayo yaliongozeka kwa asilimia 43 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2020/21.

Miongoni mwa waliokerwa na matokeo ya ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni Mh. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye aliwaambia maofisa wa serikali kwamba ‘tunaua nchi yetu wenyewe’ na ‘hautazikwa na fedha ambazo unaibia nchi yako.’ Mh. Rais pia alitoa maelekezo kwa taasisi za uwajibikaji, ikiwemo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kuhakikisha wale wote waliotajwa katika ripoti hiyo kuchunguzwa na kuwajibishwa kwa mujibu wa sheria.

Rushwa na ubadhirifu wa fedha za umma vinaathiri kwa kiasi kikubwa uwezo wa Serikali kuhakikisha utekelezaji wa haki za kijamii na kiuchumi, ikiwemo haki ya elimu, haki ya afya, na haki ya kuishi katika hali inayofaa. Fedha hizi zinazopotea sababu ya rushwa na na usimamizi mbaya, matumizi mabaya, na ubadhirifu wa fedha za umma zingeweza kutumika kuongeza bajeti za sekta muhimu kama vile elimu, afya, maji, na kilimo, ambazo zimekuwa zikishindwa kufikia viwango vya chini vya bajeti.

**Mtazamo wa LHRC:** Matokeo ya ripoti za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yanaonyesha tatizo kubwa la kutokuwepo kwa uwajibikaji wa kutosha kwa watu binafsi na taasisi za serikali linapokuja suala la fedha za umma.

**Wito wa LHRC:** Serikali kuchukua hatua kuhakikisha wale wote waliotajwa au kuhisiwa kuhusika na vitendo vya rushwa, udanganyifu, na ubadhirifu wa fedha za umma wanachunguzwa na kuchukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa sheria, ikiwemo kuondolewa katika nafasi zao.

## 4.2. Haki ya Kufurahia na Kunufaika na Rasimali Asilia

Masuala maku yaliyoathiri haki ya kufurahia na kunufaika na rasilimali asilia kwa upande wa Tanzania bara ni pamoja matukio ya rushwa na usimamizi mbaya, matumizi mabaya, na ubadhirifu wa fedha za umma yaliyoibuliwa katika Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mwak 2023.

## 4.3. Haki ya Mazingira Safi na Salama

Masuala makuu yaliyoathiri haki ya mazingira safi na salama ni pamoja na uchafuzi na uharibifu wa mazingira, kutofanya vizuri tathmini ya athari kwenye mazingira, na athari za mabadiliko ya tabianchi.

**Mtazamo wa wanajamii kuhusu uchafuzi wa mazingira**

Asilimia 79 ya wanajamii walioshiriki katika utafiti kuhusu haki za binadamu uliofanywa na LHRC katika mikoa 20 ya Tanzania Bara walisema kwamba uchafuzi wa mazingira ni tatizo katika jamii yao. Uchafuzi uliotajwa kutokea zaidi ni uchafuzi wa ardhi (asilimia 44), ukifuatiwa na uchafuzi wa maji (asilimia 39), uchafuzi wa hewa (asilimia 32), na kelele (asilmia 27).

*'Kwa kweli uchafuzi wa mazingira ni tishio kubwa hapa jijini. Ukipita mitaani unaona jinsi taka zilivyotupwa hovyo hadi mitaroni. Ukienda kwenye fukwe za public hali pia ni hivyo hivyo, basi ni tabu tu. Watu hawana mwamko wa kutunza mazingira..'*

***Msaidizi wa kisheria – Dar es Salaam***



***Taka ngumu zilizokutwa zimetupwa mtaroni Wilayani Kasulu, Kigoma (kushoto) na Jijini Dodoma, Dodoma (kulia)***

Matukio ya uchafuzi wa mazingira aina ya kelele yaliripotiwa katika mikoa kama vile Dar es Salaam, Kigoma, Dodoma, Mwanza,

Kilimanjaro, Arusha, na Mbeya. Mnamo mwezi Machi mwaka 2023, iliripotiwa kwamba kelele zimekuwa changamoto kubwa katika makazi ya watu na kwamba kelele hizo ziliwasababishia baadhi ya wakazi kupatwa na msongo wa mawazo, matatizo ya moyo, uziwi, na athari nyingine. Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) liliripoti kwamba malalamiko ya uchafuzi wa mazingira aina ya kelele na mitetemo yaliongezeka kwa asilimia 65.

NEMC iliripoti kupokea jumla ya matukio au malalmiko 317 ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira, ikiwemo kelele na mitetemo, uchafuzi wa hewa, uchafuzi wa ardhi, na uchafuzi wa maji, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23. Mnamo mwezi Mei, iliripotiwa kwamba NEMC ilifunga biashara 89 katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara kwa kusababisha uchafuzi wa mazingira.


Changamoto nyingine kubwa kwenye mazingira ni ukataji hovyo na kupita kiasi wa miti, ambayo imeonekana kuwa kubwa zaidi katika mikoa kama vile Tabora, Dodoma, Ruvuma, Pwani, Morogoro, Mbeya, na Kigoma.

*'Mkaa na kuni imelenga sana kuharibu misitu, na hilo ndio kubwa, gesi ni gharama na pia kuipata hapa ni changamoto.'*

***Mwanajamii – Bukene, Nzega***

## Uelewa kuhusu mabadiliko ya tabianchi na athari zake

Tathmini iliyofanywa na LHRC mwaka 2023 ilionyesha kwamba bado kuna changamoto ya uelewa mdogo kuhusu mabadiliko ya tabianchi na athari zake katika jamii. Miongoni mwa wanajamii waliofikiwa na LHRC, ni asilimia 21 pekee (chini ya robo) walisema wana uelewa mzuri sana (asilimia 8) na uelewa mzuri (asilimia 13) kuhusu mabadiliko ya tabianchi na athari zake. Miongoni mwa wale waliodai kuwa na uelewa mzuri sana na uelewa mzuri, karibia robo tatu (asilimia 73) walidai kuwa na wasiwasi mkubwa (asilimia 31) na wasiwasi (asilimia 42) kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi kwenye mazingira na haki za binadamu.




***%Mtazamo wa wanajamii kuhusu kuwa na wasiwasi kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi kwenye mazingira na haki za binadamu***

Mabadiliko ya tabianchi yalisababisha athari mbalimbali kwenye maisha, mazingira, na haki za binadamu mwaka 2023, ikiwemo kusababisha mafuriko, uharibifu wa nyumba na miundombinu, ukame, na kupungua kwa uzalishaji. Haki za binadamu zilizoathiriwa ni pamoja na haki ya kuishi, haki ya kuishi katika hali inayofaa (chakula na makazi), haki ya kufanya kazi, haki ya familia, haki ya afya, na haki ya maendeleo.

***'Baada ya mvua kutokua nzuri sana na kupata mazao kidogo mume wangu aliamua kuondoka kwenda kutafuta maisha mkoani Mwanza sasa ni mwaka mzima hajarudi na sasa tunaishi maisha magumu.'***

***Mwanajamii – Kasulu, Kigoma***



05

Sura ya Tano

# HAKI ZA MAKUNDI MAALUM

SURA YA TANO:

# HAKI ZA MAKUNDI MAALUM

Masuala makuu yaliyoathiri ufurahiaji wa haki za makundi maalum ni pamoja na ubaguzi na aina mbalimbali za ukatili.

## 5.1. Haki za Wanawake


Ukiacha mikataba mbalimbali ya haki za binadamu inayotoa ulinzi wa haki za binadamu kwa watu wote, kuna mikataba kadhaa ambayo ni maalum kwa ajili ya kulinda haki za wanawake. Mikataba hii ni pamoja na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW) wa mwaka 1979 na Mkataba wa Afrika wa Haki za Wanawake (Maputo Protocol) wa mwaka 2003. Jambo kubwa linalokatazwa katika mikataba hii ni ubaguzi dhidi ya wanawake - unaopelekea kushindwa kufurahia haki zao muhimu kama binadamu. Pia, mikataba hii inakataza aina zote za ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake.

### Ukatili wa kijinsia

Ukatili wa kijinsia uliendelea kuwa tishio kubwa zaidi kwa haki za wanawake. Takwimu za Dawati la Jinsia na Watoto la Jeshi la Polisi zinaonyesha kwamba jumla ya matukio 14,184 ya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto yaliripotiwa katika vituo vya polisi katika kipindi cha Mwezi Julai 2022 hadi Mei 2023, yakiongezeka kutoka matukio 12,642 katika mwaka 2021/22. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 12.2.


### Matukio ya ukatili dhidi ya wanawake yaliyoripotiwa

LHRC ilikusanya matukio 147 ya ukatili dhidi ya wanawake kupitia programu zake za ufuatiliaji wa haki za binadamu na matukio yaliyoripotiwa na vyombo vya habari pekee, yaliyoripotiwa katika mikoa karibia yote ya Tanzania Bara. Matukio haya ni 39 zaidi ya yale yaliyokusanywa mwaka 2022. Kama ilivyokuwa mwaka 2022, ukatili wa kimwili uliendelea kuchukua asilimia kubwa zaidi ya matukio ya ukatili dhidi ya wanawake (asilimia 61), ukifuatiwa na ukatili wa kingono (asilimia 20), na ukatili wa kiuchumi (asilimia 19). Wafanyaji wakuu wa vitendo hivyo vya ukatili walikuwa ni wanaume, hususan wenza, na matukio mengi yalitokea majumbani.




*% Aina ya matukio ya ukatili dhidi ya wanawake yaliyokusanywa na LHRC mwaka 2023*

LHRC ilikusanya matukio mengine 1,738 ya ukatili dhidi ya wanawake yaliyoripotiwa katika mikoa 10 kadi ya 20 ya Tanzania Bara iliyofikiwa na LHRC kupitia utafiti wake wa haki za binadamu, yakiongezeka kutoka matukio 1,391 mwaka 2022. Wahojiwa wengi mbalimbali, wakiwemo Maofisa Ustawi Mikoa na maofisa wa mashirika yasiyo ya kiserikali, walisema kwamba ukatili dhidi ya wanawake, hasa ukatili wa kimwili, uliongezeka mwaka 2023.




*Jumla ya matukio ya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya wanawake yaliyokusanywa na polisi – 2019 hadi 2023*

## Mtazamo wa jamii kuhusu ukatili dhidi ya wanawake

Takribani robo tatu ya wanajamii (asilimia 73), wakiwemo wasaidizi wa kisheria, walisema kwamba ukatili dhidi ya wanawake ni tatizo kubwa (asilimia 36) na tatizo (asilimia 37). Karibia nusu ya wanajamii (asilimia 49) walisema kwamba ukatili wa kimwili ndiyo aina kuu ya ukatili dhidi ya wanawake inayotokea katika jamii yao. Kuhusu vitendo vya ukatili vinavyotokea zaidi, wanajamii wengi walitaja kupigwa (asilimia 64), wakifuatiwa na matusi (asilimia 42), kudhalilishwa (asilimia 38), rushwa ya ngono (asilimia 25), na ubakaji (asilimia 23).

> *'Aina kuu ya ukatili wanaopitia wanawake ni vipigo, hasa kwa wale waliokuwa na mahusiano, ikiwemo wanandoa. Katika baadhi ya maeneo inaonekana ni kawaida mwanamke kupigwa na mumewe.'*
>
> ***Mwanajamii – Songea, Ruvuma***

## Matokeo ya Utafiti wa Kidemographia na afya

Ripoti ya utafiti wa kidemografia na afya iliyotolewa mwaka 2022 na Ofisi ya Taifa ya Tawimu (NBS) ilionyesha kwamba wenza wa sasa wa wanawake, wakiwemo waume, ndio wafanyaji wakuu wa ukatili wa kimwili dhidi ya wanawake (asilimia 64.4), wakifuatiwa na wenza wa zamani (asilimia 36.4). Zaidi

ya robo ya wasichana na wanawake wenye umri wa miaka 15 hadi 49 nchini Tanzania (asilimia 27) wamefanyiwa vitendo vya ukatili wa kimwili tangu wakiwa na miaka 15, huku asilimia 18 wakifanyiwa pia vitendo hivyo katika kipindi cha miezi 12 iliyopita.

### Ukatili dhidi ya mwenza

Wanawake wawili kati ya watano waliowahi kuwa na wenza nchini Tanzania wamefanyiwa ukatili dhidi ya mwenza na theluthi moja (asilimia 33) wamefanyiwa ukatili huo katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Ukatili dhidi ya mwenza uko juu zaidi katika Kanda ya Ziwa (asilimia 48.6), Kanda ya Kati (asilimia 48), Kanda ya Magharibi (asilimia 42.1), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (asilimia 41.9), na Kanda ya Kaskazini (asilimia 38.3). Kwa upande wa mikoa, mikoa sita ambayo aina hii ya ukatili ipo juu zaidi (asilimia 40 na kuendelea) ni Mara, Dodoma, Kagera, Iringa, Njombe, na Tabora.

Matukio ya ukatili dhidi ya mwenza yaliripotiwa sana mwaka 2023, ambapo LHRC ilikusanya matukio 115 kupitia njia mbalimbali, ikiwemo programu ya ufuatiliaji wa haki za binadamu na utafiti wa haki za binadamu. Mojawapo ya matokeo mabaya ya aina hii ya ukatili ni mauaji ya mwenza yanayofanywa na mwenza, ambapo kwa mwaka 2023 LHRC ilikusanya matuko 50 ya aina hii, ambayo ni 17 zaidi ya yale iliyokusanya mwaka 2022. Kati ya waliofariki sababu ya ukatili huo dhidi ya mwenza, 45 (asilimia 90) walikuwa ni wanawake na 5 (asilimia 10) wanaume. Zaidi ya asilimia 40 ya matukio hayo yalidaiwa kusababishwa na wivu wa kimapenzi.

> *'Kuna ukatili wa wanawake kupigwa mara nyingi kwa sababu ya wivu wa kimapenzi, wananigwa na waume zao, kushikwa koromeo, wengine mpaka wanaumwa kwa sababu ya kushikwa koromeo.'*
>
> ***Mwanajamii (machinga) – Nzega, Tabora***

### Ukatili wa kisaikolojia dhidi ya wanawake

Ukatili wa kisaikolojia pia uliendelea kuwa changamoto kwa wanawake mwaa 2023. Vitendo vya aina hii ya ukatili kama vile matusi, udhalilishaji, utelekezaji viliripotiwa katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara.

### Ukatili wa kingono dhidi ya wanawake

Ukatili wa kingono ni tishio kubwa kwa afya ya akili na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu. Nchini Tanzania, asilimia 12 ya wasichana na wanawake wenye umri wa miaka 15 hadi 49 wamewahi kufanyiwa ukatili wa kingono na mtu yeyote, ikishuka kutoka asilimia 17 mwaka 2015. Hii ni kwa mujibu wa matokeo ya utafiti wa kidemografia na afya uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu mwaka 2022. Mikoa inayoongoza kwa kuwa

na waathirika wengi zaidi wa ukatili wa kingono (iliyopata asilimia 20) ni Kagera, Mwanza, na Mara, huku Mkoa wa Mtwara ukiwa na asilimia ndogo zaidi (asilimia 1). Tathmini ya matukio ya ukatili dhidi ya wanawake yaliyokusanywa na LHRC mwaka 2023 inaonyesha kwamba asilimia 20 ya matukio hayo ilikuwa ni ukatili wa kingono.

LHRC ilikusanya zaidi ya matuio 300 ya ukatili wa kingono dhidi ya wanawake mwaka 2023, ikiwemo matukio ya ubakaji, jaribio la ubakaji, udhalilishaji au unyanyasaji wa kingono, rushwa ya ngono, ulawiti, na ubakaji mande. LHRC imegundua kwamba changamoto ya ubakaji kwa wanawake wazee inachangiwa na imani za kishirikina. Mwaka 2023 pia ulishuhudia mjadala wa ubakaji na ulawiti ndani ya ndoa kuendelea katika majukwaa mbalimbali, huku wanaharakati na watetezi wa haki za wanawake wakiendelea kudai marekebisho ya sheria ili kuvifanya vitendo hivyo vya ukatili kuwa kosa la jinai.

## Ukatili wa kiuchumi dhidi ya wanawake

Matikuo ya ukatili wa kiuchumi dhidi ya wanawake, ikiwemo kunyimwa haki za kumiliki na kurithi mali, utoaji kinguvu wa wajane katika nyumba zao, na mwanamke kutoruhusiwa kutumia kipato (fedha) cha familia, yaliripotiwa pia kwa wingi kiasi mwaka 2023. LHRC ilikusanya matukio 323 ya aina hii ya ukatili dhidi ya wanawake. Mojawapo ya visababishi vikuu vya ukatili huu ni mila na desturi baguzi.

*'Umiliki wa mali kwa mila zetu hazitambui kuwa naye anaweza au ana haki ya kumiliki mali,hivyo ndivyo iwapelekea wajane kukataziwa kumiliki mali baada ya wanaume kufa.'*

***Msaidizi wa kisheria – Kongwa, Dodoma***

## Ukatili dhidi ya wanawake mtandaoni

Ukatili dhidi ya wanawake mtandaoni pia umekuwa changamoto kubwa kwa wanawake nchini Tanzania, kama ilivyo katika nchi nyingine nyingi duniani. Takribani theluthi mbili ya wanajamii waliofikiwa na LHRC mwaka 2023 (asilimia 62) walisema kwamba aina hii ya ukatili ni tatizo (asilimia 34) na tatizo kubwa (asilimia 28). Matusi yalitajwa kama kitendo cha ukatili dhidi ya wanawake mtandaoni kinachofanywa zaidi (asilimia 47), yakifuatiwa na matumizi ya picha ya mtu ya faragha mtandaoni bila ridhaa yake (asilimia 31). LHRC ilikusanya matukio 22 ya ukatili dhidi ya wanawake mtandaoni, hasa ya matumizi ya picha ya mtu ya faragha mtandaoni bila ridhaa yake, yaliyoripotiwa katika baadhi ya mikoa iliyotembelewa mwaka 2023. Watuhumiwa wengi wa ukatili huo walikuwa ni wapenzi wa zamani na sasa wa wanawake hao, huku baadhi yao wakiwashuritisha wanawake

kuwapatia pesa au kuendelea kuwa na uhusiano nao wa kimapenzi ili wasisambaze picha na video zao za utupu.

*'Mchumba wa dada yangu kakataa kumuoa dada sababu kuna mwanaume aliingia kwenye profile ya dada ya mtandao wa facebook akachukua picha za dada akapakua na kisha akaziedit picha za dada na baadae akazipost kwenye ukurasa wake dada akiwa mtupu.'*


***Kijana wa kike – Kasulu, Kigoma***

## Changamoto kuu katia kupambana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto

Changamoto kuu katia mapambano dhidi ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto ni pamoja na mila na desturi baguzi, upungufu mkubwa wa maofisa ustawi wa jamii, ufinyu wa bajeti, ukatili dhidi ya wanawake na watoto kuchukuliwa kama jambo la kawaida katika jamii, ulevi, uratibu duni, na ufanisi mdogo wa kamati za kupambana na kuzuia ukatili huo (MTAKUWWA).

*'Pale tunapokosea lazima tupigwe na waume zetu ili kutuweka sawa, ni haki yao kutupiga.'*

***Mwanamke – Kibondo, Kigoma***




***% Uhusiano kati ya ukatili dhidi ya mwenza na matumizi ya pombe***
***Chanzo: TDHS-MIS 2022***

## Ushiriki wa wanawake katika siasa

Vikwazo mbalimbali vya Kiuchumi na kijamii viliendelea kuzuia ushiriki madhubuti wa wanawake katika siasa mwaka 2023. Vikwazo hivyo ni pamoja na mianya ya kijinsia katika sheria za uchaguzi na vyama vya siasa kama vile Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sheria ya Vyama vya Siasa, na Sheria ya Taifa ya Uchaguzi. Mila na destruri baguzi ziliendelea kuwa mwiba kwa ushiriki wa wanawake katika siasa katika baadhi ya jamii Tanzania Bara. Pia, ukatili dhidi ya wanawake wanasiasa, wanawake wanasiasa kutopewa msaada na ushirikiano wa kutosha ndani ya vyama vya siasa, sambamba na kutokuwa na uwakilishi mzuri katika vyombo vya ufanyaji maamuzi, ni miongoni mwa changamoto ambazo bado zipo wakati nchi ikielekea kwenye chaguzi za mwaka 2024 na 2025.

### Upatikanaji na ufikiaji wa haki kwa wanawake

Wanawake pia wanakumbana na changamoto mbalimbali ambazo zinakuwa vikwazo kwao katika kufikia na kupata haki. Vikwazo hivyo ni pamoja na kutojua mahala pa kutoa malalamiko, umaskini na gharama kubwa za uwakilishi wa kisheria, mfumo dume, uelewa mdogo kuhusu sheria, rushwa, mila na desturi baguzi, na upatikanaji hafifu wa huduma za msaada wa kisheria.


## 5.2. Haki za Watoto

Haki za watoto zinalindwa katika mikataba mikubwa miwili ya haki za watoto, ambayo ni: Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto (CRC) wa mwaka 1989 na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (ACRWC) wa mwaka 1990, yote ikiwa imeridhiwa na Tanzania. Kwa hapa nchini Tanzania pia tuna Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 ambayo inataja haki za msingi za mtoto kama zilivyoelezewa kwenye mikataba hiyo na kueleza wazi kwamba katika kufanya maamuzi yoyote kuhusu mtoto kanuni ya maslahi bora ya mtoto lazima izingatiwe. Mikataba hii na sheria ya mtoto inatoa wajibu kwa Serikali, wazazi, walezi na wanajamii kwa ujumla kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vyote vya ukatili na ubaguzi.

### Mienendo ya ukatili dhidi ya watoto na mahala ukatili huo unapotokea

Ukatili dhidi ya watoto uliendelea kuwa mojawapo ya changamoto kuu kwa haki za watoto nchini Tanzania mwaka 2023. Uchakataji wa takwimu na data za Jeshi la Polisi za vitendo vya ukatili dhidi ya watoto vilivyoripotiwa katika miaka ya hivi karibuni unaonyesha kwamba zaidi ya matukio 30 ya ukatili dhidi ya watoto hutokea kila siku nchini Tanzania, na zaidi ya theluthi mbili ya manusura (watoto 8 kati ya 10) ni wasichana. Katika kipindi cha Mwezi Janauri 2022 hadi Machi 2023, jumla ya matukio ya ukatili dhidi ya watoto 15,901 yaliripotiwa vituoni vya polisi.


Mwaka 2023 iliripotiwa kwamba asilimia 60 ya matukio ya ukatili dhidi ya watoto hutokea nyumbani, huku asilimia 40 iliyobakia ikitoea sehemu nyingine kama vile mitaani na shuleni.




***Manusura wa ukatili dhidi ya watoto nchini Tanzania kwa umri – 2019 hadi 2023***
***Chanzo: Takwimu za polisi, 2019 to 2023***

## Matukio ya ukatili dhidi ya watoto yaliyoripotiwa

Baadhi ya watoto katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara waliendelea kufanyiwa aina mbalimbali za ukatili, ikiwemo wa kimwili, kingono, kisaikolojia, na kiuchumi. LHRC ilikusanya jumla ya matukio 464 ya ukatili dhidi ya watoto, yakiongezeka kutoka matukio 350 mwaka 2022. Ukatili wa kingono uliendelea kuongoza (asilimia 79), ukifuatiwa na ukatili wa kimwili na kisaikolojia (asilimia 19), na ukatili wa kiuchumi (asilimia 2). Miongoni mwa waliofanyiwa vitendo hivyo vya ukatili ni watoto wenye umri mdogo wa mwaka mmoja na wafanyaji wa vitendo hivyo walijumuisha wazazi, ndugu wa karibu, watoto wengine, walimu, majirani, na watu wasiofahamika.




***%Aina ya matukio ya ukatili dhidi ya watoto yaliyokusanywa na LHRC mwaka 2023***


*'Matendo mengi ya ukatili yanatokea kwa watu ambao tunaukaribu katika jamii hivyo tunapata uoga kwenda katika mamlaka kwa hofu ya kuleta migogoro katika jamii zetu lakini ni vitendo vinavyotakiwa kupigwa vita usiku na mchana.'*


***Mwanajamii – Bumbuli, Tanga***

**Ukatili wa kingono,** hasa vitendo vya ubakaji na ulawiti, uliendelea kuwa aina ya ukatili dhidi ya watoto inayotokea zaidi katika jamii. Wafanyaji wa vitendo hivyo vya ukatili wa kingono dhidi ya watoto walijumuisha baba wa kambo, ambapo mojawapo ya sababu za kufanya vitendo hivyo vya kinyama ilikuwa ni kufuata maelelekezo ya waganga wa kienyeji ili kupata utajiri. Zaidi ya asilimia 80 ya manusura wa ubakaji ni wasichana, huku wavulana wakiwa ni asilimia 87 ya manusura wa vitendo vya ulawiti.

## Ubakaji

Wasichana waliendelea kuwa manusura wakuu wa vitendo vya ubakaji nchini Tanzania. Jumla ya matukio 57,335 ya ubakaji yaliripotiwa nchi nzima katika kipindi cha miaka ya 2015 hadi 2022. Hii ni sawa na wastani wa matukio 7,166 kila mwaka na 597 kila mwezi.




***Matukio ya ubakaji yaliyoripotiwa nchini Tanzania – 2015 hadi 2023***
***Chanzo: NBS & TPF***

**Matukio ya ukatili** wa kimwili pia yaliripotiwa katia maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara. Watoto walifanyiwa vitendo mbalimbali vya ukatili, ikiwemo vipigo, kuchomwa sehemu mbalimbali za mwili, utesaji, ubakaji, jaribio la ubakaji, rushwa ya ngono, unyanyasaji wa kingono, udhalilishaji, na matusi. Wafanyaji wa vitendo hivyo vya ukatili walijumuisha wazazi, babu na bibi, wajomba, ndugu, walimu, na watu wasiofahamika.

Takribani robo (asilimia 23) ya matukio ya ukatili wa kimwili dhidi ya watoto yaliyokusanywa na LHRC mwaka 2023 yalijumuisha adhabu ya kuwachoma watoto katika sehemu mbalimbali za miili yao, ikiwemo mikono.

## Adhabu yenye kusababisha madhara ya kimwili

Adhabu zenye kusababisha madhara ya kimwili, ikiwemo adhabu kali ya viboko, zilizendelea kuwa tishio kwa ustawi wa kimwili na kihisia wa watoto katika maeneo ya shule na nyumbani. LHRC iliusanya matukio 11 ya adhabu zenye kusababisha madhara ya kimwili, ikiwemo adhabu kali za viboko, yaliyoripotiwa katika Mikoa ya Kilimanjaro, Mbeya, Dar es Salam, Morogoro, Kagera, Kigoma, na Dodoma. Mbali na kusababisha madhara ya kimwili, baadhi ya matukio hayo yamekuwa yakipeleea vifo vya watoto. Mathalani, katika kipindi cha mwaka 2018 hadi 2023, LHRC imekusanya jumla ya vifo nane vya watoto vilivyosababishwa na adhabu kali iliyotolewa na walimu shuleni. Pia, kumekuwa na matukio kadhaa ya wazazi kuwapiga na kuwasababishia umauti watoto wao.

Ukatili wa kisaikolojia dhidi ya watoto, hasa

utelekezaji wa watoto, pia ulendelea kuwa mojawapo ya changamoto kubwa kwa ustawi wa watoto. Changamoto nyingine ni pamoja na ajira za watoto na utumikishwaji wa watoto. Maofisa Ustawi wa Jamii na maofisa wa mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali kutoka mikoa 20 ya Tanzania Bara waliohojiwa mwaka 2023 walisema kwamba matukio ya utelekezaji wa watoto na famila yamekuwa yakitokea mara kwa mara.

### Mtazamo wa jamii kuhusu ukatili dhidi ya watoto

Kama ilivyokuwa mwaka 2022, zaidi ya theluthi mbili ya wanajamii (asilimia 77) walisema kwamba ukatili dhidi ya watoto ni tatizo (asilimia 39) na tatizo kubwa (asilimia 38).

> *'Ukatili wa watoto nadhani ndo upo mwingi kuliko hata ukatili wa wanawake.'*
>
> ***Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa – Singida***

### Ukatili wa kingono dhidi ya watoto unaofanywa watoto na ukatili wa kingono dhidi ya wavulana

Matukio ya watoto kuwafanyia ukatili wa kingono watoto wenzao pamoja na yale ya watoto wa kiume kufanyiwa ukatili wa kingono yaliripotiwa kwa wingi katika maeneo mbalimbali mwaka 2023. LHRC ilikusanya matukio 87 ya watoto wa kiume kufanyiwa ukatili wa kingono (ulawiti), ambayo ni matukio 79 pungufu ya yale iliyokusanya mwaka 2022. Hata hivyo matukio hayo ni sehemu ndogo tu ya matukio yanayotokea katika jamii, kwani kwa wastani, matukio ya ulawiti 900 huripotiwa vituo vya polisi kila mwaka na zaidi ya asilimia 80 ya wanaofanyiwa unyama huo ni wavulana.

> *'Kuna mwanaume alilawiti watoto watatu. Watoto hao walikuwa wanachunga ngo'mbe wakaingiza shambani kwake, akasema adhabu yake ni kuwalawiti, akaanza na mmoja alivyofika wa tatu akaishiwa nguvu akaripotiwa serikali za mtaa.'*
>
> ***Mkurugenzi asasi ya kiraia – Tabora***

Mkoani Dar es Salaam, iliripotiwa mnamo Mwezi Julai mwaka 2023 kwamba watoto wengi ambao wanapelekwa mahakama za watoto mkoani humo wanatuhumiwa kuwafanyia wenzao kitendo cha ulawiti, na kwamba hii inachangiwa na malezi duni, msukumo rika, na umaskini wa kipato ndani ya familia.

### Ndoa na mimba za utotoni

Ndoa na mimba za utotoni ziliendelea kuwa mwiba na kikwazo cha ustawi kwa wasichana mwaka 2023. LHRC ilikusanya matukio 14 ya

ndoa za utotoni, ambayo ni mawili pungufu ya yale iliyokusanya mwaka 2022. Mahari iliendelea kutajwa kama kichocheo kikuu cha ndoa za utotoni. Vichocheo vingine ni pamoja na ndoa za utotoni kuonekana kama jambo la kawaida, ukeketaji, mila na desturi baguzi, utelekezaji, na mianya katika ulinzi wa kisheria wa haki za wasichana. Mojawapo ya mianya katika sheria ni Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, ambayo inaruhusu watoto kuolewa.

***'Hapa Igunga mwaka huu 2023 katika kata ya Ziba kuna familia moja waliolewa mapacha ambao ni wadogo wamemaliza tu darasa la saba, baada ya kupanga mahari kwa pacha mmoja, kaka mtu nae akaoa yule pacha mwingine. Mama alilia sana, alikuwa mjamzito, ikafika mahali akajifungua kabla ya muda.'***

***Mkurugenzi asasi ya kiraia – Nzega, Tabora***

Utafiti wa Kidemografia na Afya na Kiashiria cha Malaria uliofanyika mwaka 2022 unaonyesha kwamba asilimia 22 ya wasichana wenye umri wa miaka 15 hadi 19 nchini Tanzania wamewahi kupata ujauzito na asilimia 6 wana ujauzito kwa sasa. Mimba za utotoni zimekithiri zaidi katika Mikoa ya Songwe (asilimia 44.7), Ruvuma (asilimia 37.2), Katavi (asilimia 34.4), Mara (asilimia 31.1), Rukwa (asilimia 29.6), Tabora (asilimia 29.1), Manyara (asilimia 28.8), Geita (asilimia 28.4), Morogoro (asilimia 28.0), na Mtwara (asilimia 25.7). Kwa mwaka 2023, matukio ya mimba za utotoni yaliripotiwa katika maeneo mbalimbali, ambapo LHRC ilikusanya matukio 2,953 yaliyoripotiwa katika mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara.

### Ukeketaji

Takwimu za serikali zimeonyesha ukeketaji kupungua nchini. Mathalani, ukeketaji umepungua kutoka asilimia 18 mwaka 1996 hadi asilimia 8 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 10. Kwa sasa mikoa inayoongoza kwa ukeketaji ni Manyara (asilimia 43), Arusha (asilimia 43), Mara (asilimia 28), Singida (asilimia 20), Tanga (asilimia 19), Dodoma (asilimia 18), na Iringa (asilimia 12).

***'Ukeketaji umeshuka ila sio kwamba haupo, sema sasa hivi unafanyika kwa siri kubwa mno. Kama bangi.'***

***Ofisa asasi ya kiraia – Manyoni, Singida***

### Usafirishaji haramu wa watoto

Usafirishaji haramu wa watoto ni mojawapo ya vikwazo vikuu vya ulinzi na usalama wa watoto. Kwa mwaka 2023, LHRC ilikusanya matukio 15 ya usafirishaji haramu wa binadamu, ambapo matukio 11 (asilimia 73), yalikuwa ni ya usafirishaji haramu wa

watoto. Mnamo Mwezi Mei 2023, Waziri wa Mambo ya Ndani, Mh. Hamad Masauni (MB), aliliambia Bunge kwamba, kwa kushirikiana na wadau wengine, wizara yake iliwaokoa manusura 190 wa usafirishaji haramu wa binadamu, ambapo asilimia 73 walikuwa ni watoto.

## Changamoto katika mapambano dhidi ya ukatili dhidi ya watoto

Changamoto katika mapambano dhidi ya ukatili dhidi ya watoto ni pamoja na kutokuwepo kwa ulinzi wa kutosha kisheria wa watoto; rushwa, hasa pale ambapo wafanyaji wa vitendo vya ukatili hutoa rushwa kwa wazazi au walezi; upungufu wa nyumba salama na familia za kuwahifadhi watoto wanaofanyiwa vitendo vya ukatili; na utamaduni wa kukaa kimya, kusamehe, na 'kuficha aibu ya familia.'

*'Imekuwa kawaida kwa watuhumiwa wa ukatili dhidi ya watoto, hasa ukatili wa kingono, kujaribu kutoa rushwa ili kujiondoa katia matatizo wasifungwe, na wazazi wanashawishika kukubali sababu ya umaskini.'*

***Mwanajamii - Dar***

## Ajira kwa watoto na utumikishwaji wa watoto

Kwa mwaka 2023, LHRC ilikusanya matukio 33 ya ajira kwa watoto na utumikishwaji wa watoto, ambayo ni 13 zaidi ya yale iliyokusanya mwaka 2022. Matukio hayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Tanga, Arusha, Dodoma, Morogoro, Tabora, Kilimanjaro, Rukwa, na Kigoma.



***Watoto ambao walikutwa wanafanya kazi katika mgodi katika Kata ya Lusu wilayani Nzega***

Ni kawaida kuwaona watoto wakifanya kazi kama wachuuzi mitaani katika mikoa mingi, hasa maeneo ya mijini, wakifanya kazi hiyo wakati ambao walitakiwa kuwa shuleni wakisoma. Watoto wengi wamekuwa wakitumia masaa mengi mtaani wakifanya kazi hizo katika mazingira magumu.

*'Ajira kwa watoto zina madhara makubwa kwenye elimu kwa sababu utakuta mtoto anaenda shule siku tatu, siku mbili haendi anaenda kwenye ajira.'*

***Ofisa Maendeleo ya Jamii – Morogoro***

## 5.3. Haki za Watu wenye Ulemavu

Masuala makuu yaliyoathiri haki za watu wenye ulemavu mwaka 2023 ni pamoja na changamoto ya upatikanaji ajira na fursa za kiuchumi, ikiwemo ubaguzi katika ajira; na unyanyapaa na ubaguzi kwa ujumla. Wanajamii walioshiriki katika utafiti wa LHRC walitaja unyanyapaa na ubaguzi kama changamoto kubwa zaidi wanayokabiliana nayo watu wenye ulemavu (asilimia 48), ikifuatiwa na umaskini na kutokuwa na kipato cha uhakika (asilimia 44) na miundombinu isiyo rafiki (asilimia 42).

*'Changamoto kubwa ya watu wenye ulemavu ni ubaguzi, tunaonekana tunayaweza yale ya kilemavu lemavu tu.'*

***Mkurugenzi wa asasi ya kiraia – Tabora***

Mojawapo ya dhana potofu kuhusu watu wenye ulemavu ambayo LHRC ilitambua katika mikoa mbalimbali iliyoitembelea mwaka 2023 ni dhana kwamba wanawake wenye ulemavu hawatakiwi kubeba ujauzito kwa sababu ya hali waliyonayo.

*"Manesi wengi huwaambia kuwa nyie hamjionei huruma na hali zenu bado mnakwenda kubeba mimba.'*

***Mtu mwenye ulemavu – Mbeya***

Watoto wenye ulemavu pia waliendelea kufanyiwa vitendo vya unyanyapaa na ubaguzi, ikiwemo shuleni. LHRC pia ilibaini kwamba baadhi ya wazazi katika mikoa iliyotembelea mwaka 2023 hawakuwa na imani na watoto wao wenye ulemavu na kuona kwamba siyo lazima kuwapeleka shule. Hii imepelekea kukithiri kwa utelekezaji wa watoto wenye ulemavu, ambao ni ukatili wa kisaikolojia, katika baadhi ya mikoa hiyo.

*'Watoto wengi wenye ulemavu wanatelekezwa na wazazi wao na kuwaacha watoto hao kwa bibi zao na huwaona kama mizigo na hawana faida.'*

***Ofisa asasi ya kiraia - Kilimanjaro***

Changamoto nyingine ambazo watu wenye ulemavu wanakumbana nazo ni pamoja na uelewa mdogo kuhusu haki zao; ufikiaji na upatikanaji wa haki; miundombinu isiyo rafiki; usafirishaji haramu, hasa kwa ajili ya kuomba; na ufikiaji wa huduma bora za elimu na afya.

## 5.4.Haki za Wazee

Masuala makuu yaliyobainika kuathiri haki za wazee nchini mwaka 2023 ni pamoja na aina tofauti za ukatili, ambazo zinaathiri usalama na ustawi wao; upatikanaji wa huduma za afya; mauaji; na ulinzi wa kijamii. Wanajamii walioshiriki katika utafiti kuhusu haki za binadamu uliofanywa na LHRC katika mikoa

mbalimbali ulibainisha umaskini na kutokuwa na kipato cha uhakika kama changamoto kubwa zaidi ambayo wazee wanakabiliana nayo (asilimia 57), ikifuatiwa na upatikanaji wa huduma bora za afya (asilimia 45), upungufu wa chakula (asilimia 40), kulazimika kulea wajukuu (asilimia 38), na kutelekezwa/kutengwa (asilimia 36). Wazee mbalimbali waliohojiwa kwa kina pia walitaja upatikanaji wa hudumua bora za afya kama changamoto kubwa kwao, wakilalamika kuhusu huduma za afya wanazotakiwa kupewa bure kutotolewa ipasavyo.

> *'Kuna wakati tunapata vipimo bure lakini ukienda kwenye dirisha la dawa unatakiwa kununua…Bila hivyo utapewa dawa za kutuliza maumivu tu kama vile panaldo hizi kwa kiasi kikubwa wanatoa bure.'*
>
> ***Mzee – Bumbuli, Tanga***

Baadhi ya wazee walifanyiwa vitendo mbalimbali vya ukatili, ikiwemo ukatili wa kimwili, kingono, kiuchumi, na kisakolojia. LHRC ilikusanya matukio 24 ya ukadili dhidi ya wazee mwaka 2023. Miongoni mwa matukio hayo ni yale ya wazee kushambuliwa na wengine kuuawa kwa sababu ya tuhuma za uchawi, huku wengine wakishambuliwa au kuuawa na watoto wao kwa sababu ya mali, wakidai urithi.

> *'Wazee wengi wanaouawa kwa sababu za kishirikina ni wanawake kwa sababu wanawake ndio wanaopika kwa kutumia kuni au mkaa, hivyo kuwa na macho mekundu.'*
>
> ***Mshiriki wa majadiliano – Igunga, Tabora***

Wazee pia walitaja ukosefu wa ulinzi wa kutosha wa kijamii, ikiwemo kutokuwepo kwa pensheni ya kila mwezi kwa wazee wote, kama changamoto. Wengi wao waliiomba Serikali kutunga sheria ya ulinzi wa wazee, kama ilivyo kwa upande wa Zanzibar. Mwaka 2017 Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania ilipendekeza kutungwa kwa sheria ya wazee, ambayo, pamoja na mambo mengine, itaanzisha mpango wa utoaji pensheni kwa wazee.

**Wito wa LHRC:** Serikali ichukue hatua ya kutunga sheria ya ulinzi wa wazee, ambayo, pamoja na mambo mengine, itaanzisha mpango wa utoaji pensheni kwa wazee.

Changamoto nyingine ambayo wazee walisema wanakumbana nayo mwaka 2023 ni kuachiwa mzigo wa kulea wajukuu zao na watoto wao. Wazee hao walilamika kuachiwa jukumu la kulea wajukuu bila msaada wowote au msaada wa kutosha, ili kutimiza mahitaji ya wajukuu zao. Matukio ya aina hii yaliripotiwa katika mikoa mbalimbali, hasa

Singida, Rukwa, Kigoma, Njombe, na Pwani.

> ***‘Tatizo la watoto kuwaachia wazee wao wajukuu wawalee bina msaada wowote limekuwa kubwa katika jamii yetu.’***
>
> ***Mwanajamii – Njombe***

## 5.5. Haki za Vijana

Kama ilivyo kwa vijana wengine katika sehemu mbalimbali duniani, barani Afrika vijana pia wana mkataba mahsusi kwa ajili yao, uitwao Mkataba wa Vijana wa Kiafrika wa mwaka 2006. Kwa mujibu wa mkataba huu, kijana ni mtu yeyote mwenye umri wa miaka kati ya 15 na 35.

Kwa mwaka 2023 mahojiano na vijana na uchambuzi wa nyaraka mbalimbali ulionyesha kwamba changamoto kuu wanazokumbana nazo vijana kwa upande wa Tanzania Bara ni pamoja na ukosefu wa ajira; upatikanaji wa elimu bora; afya ya akili; upatikanaji wa huduma bora za afya; ukatili, hasa kwa vijana chini ya miaka 18; na uwakilishi katika ufanyaji maamuzi.

Uchambuzi wa matukio ya ukatili yaliyoripotiwa mwaka 2023 pamoja na takwimu za utafiti wa kidemografia na afya unaonyesha kwamba watu wengi waliofanyiwa vitendo vya ukatili walikuwa ni vijana (miaka 15 hadi 35), hasa watoto (wasichana na wavulana) na vijana wa kike.

Matatizo ya afya ya akili miongoni mwa vijana yanachangiwa na ukatili na ukosefu wa ajira. Changamoto hizi na nyingine hupelekea vijana kupatwa na msongo wa mawazo, wasiwasi, na sonona (huzuni iliyopitiliza), na hivyo kuongeza uwezekano wa vijana hao kujiingiza katika vitendo vya kihalifu na matumizi ya madawa.

## 5.6. Haki za Watu Wanaoishi na VVU

Kwa mwaka 2023, unyanyapaa na ubaguzi viliendelea kuwa changamoto kuu kwa watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (VVU) nchini Tanzania. Kwa mujibu wa utafiti wa kidemografia na afya wa mwaka 2022, asilimia 28 ya wasichana na wanawake na 27 ya wavulana na wanaume wenye miaka 15 hadi 49 wana mitazamo ya kibaguzi dhidi ya watu wanaoishi na VVU. Mitazamo hiyo ya kibaguzi ipo zaidi vijijini ukilinganisha na mijini, na hupungua kadri elimu ya mtu inapoongezeka. Unyanyapaa na ubaguzi wa watu wenye VVU unaathiri utayari wa watu kupima VVU na kuzingatia matumizi ya dawa za kufubaza virusi hivyo.



06

Sura ya Sita

# VYOMBO VYA ULINZI WA HAKI ZA BINADAMU

SURA YA SITA:

# VYOMBO VYA ULINZI WA HAKI ZA BINADAMU

## 6.1.Vyombo vya Kitaifa vya Ulinzi wa Haki za Binadamu

Vyombo vya ulinzi wa haki za binadamu nchini Tanzania vinajumuisha vyombo kama vile Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mhimili wa Mahakama, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Jeshi la Polisi Tanzania, na Jeshi la Magereza.

Pamoja na juhudi mbalimbali za kukuza na kulinda haki za binadamu nchini Tanzania, mifumo hii iliendelea kukabiliwa na chamoto mbalimbali, ikiwemo upungufu wa wafanyakazi; ucheleweshaji katika upelelezi na ukamilishaji wa kesi; rushwa; mianya katika uwezo wa utendaji kazi, hasa kwa upande wa upelelezi; mianya katika ufuatiliaji na tathmini; ufinyu wa bajeti; na mazingira duni ya kazi, hasa kwa upande wa polisi.

## 6.2.Vyombo vya Kikanda na Kimataifa vya Ulinzi wa Haki za Binadamu

Masuala makuu yaliyoathiri nafasi ya mifumo ya kikanda na kimataifa ya haki za binadamu katika kulinda haki za binadamu nchini ni pamoja na Tanzania kuondoa ruhusa ya watu binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali kufungua kesi kwa niaba ya watu katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Watu na Binadamu na kutotekelezwa kwa hukumu na mapendekezo ya mifumo hiyo katika kesi mbalimbali zilizofunguliwa dhidi ya Tanzania.



07


Sura ya Saba

# UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO

SURA YA SABA:

# UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO

Kwa mwaka 2023, asilimia ya mapendekezo yaliyotolewa na LHRC katika ripoti zilizopita ambayo yalitekelezwa ilikuwa asilimia 36, ikiongezeka kutoka asilimia 35 mwaka 2022. Asilimia ya mapendekezo yaliyotekelezwa kiasi pia iliongezeka kutoka asilimia 38 mwaka 2022 hadi asilimia 40 mwaka 2023, huku asilimia ya mapendekezo ambayo hayajatekelezwa kabisa ikipungua kutoka asilimia 26 mwaka 2022 hadi asilimia 23 mwaka 2023.




*Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ripoti za haki za binadamu za (2015 – 2022)*

**Wito wa LHRC:** Ili kuimarisha ulinzi wa haki za msingi za binadamu, usawa wa kijamii, na ufikiaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu, tunaisihi Serikali na wadau wengine kutekeleza mapendekezo ambayo bado hayajatekelezwa na yale ambayo hayajatekelezwa kikamili



LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

LHRC

KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Are you passionate about the protection and promotion of Human Rights?

## Donate Now!

airtel money

### How to Donate (Airtel Money)

1st Step: Dial *150*60# to access your AIRTEL MONEY account.
2nd Step: Select 5 – Make Payments.
3rd Step: Select 4 – Enter Business Number.
4th Step: Enter business number (275454)
5th Step: Enter the amount you want to pay.
6th Step: Enter the reference number.(1234)
7th Step: Enter your "PIN" to confirm.

tigo pesa

### How to Donate (TigoPesa)

1st Step: Dial *150*01 # to access your Tigo Pesa account.
2nd Step: Select 4 – Pay Bills.
3rd Step: Select 3 – Enter Business Number.
4th Step: Enter business number (275454)
5th Step: Enter the reference number.(1234)
6th Step: Enter the amount you want to pay.
7th Step: Enter your "PIN" to confirm.

vodacom m-pesa

### How to Donate (M-PESA)

1st Step: Dial *150*00# to access your MPESA account.
2nd Step: Select 4 – Pay By Mpesa.
3rd Step: Select 4 – Enter Business Number.
4th Step: Enter Business number (275454)
5th Step: Enter the reference number.(1234)
6th Step: Enter the amount you want to pay.
7th Step: Enter your "PIN" to confirm.
8th Step: Enter 1 to confirm the transaction

@humanrightstz You Tube Haki TV

*For a Just and Equitable Society*



**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU (MAKAO MAKUU)**
Jengo la Jaji Lugakingira,
S. L. P. 75254, Kijitonyama, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz **Tovuti:** www.humanrights.or.tz

**KITUO CHA MSAADA WA SHERIA**
Mtaa wa Isere - Kinondoni, S. L. P. 79633, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 22 2761205/6 **Barua Pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

**OFISI YA ARUSHA**
Barabara ya Olerian, Olosiva, Kitalu Na. 116/5, Sakina kwa Idd,
S. L. P. 15243, Arusha – Tanzania
**Simu:** +255 27 2544187 **Barua Pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**OFISI YA DODOMA**
Kitalu na 22. Area D, S.L.P 2289, Dodoma, Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 262350050 **Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

@humanrightstz HakiTV